BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,018,116,895/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**Tanzania** yazidi kung'ara medani ya kimataifa


LATRA mnaupiga wote, lakini pigeni na hapa
Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA JULAI 29, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

TARURA yahesabu orodha ya mafanikio kwa miaka mitano kuanzishwa kwake
Ukurasa 12

Na Shaban Njia, KAHAMA

**Tanesco yaanza mpambano na wezi vifaa Shinyanga kupitia Sungusungu**
• Wajibiwa kazi inaanza mara moja

MKOA wa Shinyanga hususani wilaya ya Kahama inatajwa kuwa kinara wa kuharibu miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hasa wizi wa mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma katika kanda ya Magharibi, ambapo pia kuna mikoa kama vile Tabora, Katavi na Kigoma.

Ni hali ambayo zao lake ni wateja wa Tanesco kuendelea kukosa huduma kwa wakati, viwanda kusimamisha uzalishaji kwa muda usiojulikana, huku shirika hilo nalo mapato yake yakididimia mkoani humo.

Pia, ni wizi unaokwamisha juhudi za shirika kusogeza huduma ya nishati kwa wananchi, hususani kwa wanaoishi pembezoni mwa miji na miradi yao nayo, haikamiliki kwa wakati.

Hapo ndipo Tanesco Kahama, imeamua kushirikisha askari wa jadi, Sungusungu kuchukua jukumu la kulinda miundombinu ya umeme katika maeneo yao, kuwadhibiti wezi wanaohujumu shirika, wakienda kuuza vitu hivyo kama vyuma chakavu.

Sungusungu hao ni kutoka kata 58 za Halmashauri za Msalala, Ushetu, na Manispaa ya Kahama, pale wanapomuona mtu au fundi anapanda kwenye nguzo za umeme, wahakikishe wanamhoji kujua uhalali wake, pia penye shaka watoe taarifa katika ofisi za Tanesco kujiridhisha.

Ofisa wa Shirika la Tanesco wilayani Kahama, Mhandisi Iddi A. Iddi, akiwaonyesha Sungusungu nyaya aina ya kopa zinazoibiwa zaidi kwenye transfoma. PICHA: SHABAN NJIA.

**OFISA KANDA YA MAGHARIBI**

Ofisa Usalama Kanda ya Magharibi Tanesco, Mhandisi Saidi Songwe, wilaya ya Kahama imekuwa kinara wa kuhujumu miundombinu za umeme, wakiiba mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma, hata kulifikisha shirika hilo kupata hasara ya Sh. milioni 400 hadi sasa.

Anasema hata wateja wao, nao wanaendelea kukosa huduma kwa matumzi ya kawaida na uzalishaji, huku Tanesco inakosa kwa kiasi kikubwa, kutokana na kuhujumiwa vifaa ambavyo ndivyo ulinzi mkubwa wa tansfoma.

Mhandisi Songwe anafafanua, yanapotolewa mafuta na anachokita 'nyaya za kopa' kwenye transfoma, Tanesco huingia gharama ya Sh.milioni 12 kurekebisha na inapochelewa, hasara ni huwa maradufu, akitoa mfano wa pigo la hasara, Sh.milioni 400 na ndiyo sababu ya kushirikisha Sungusungu kuimarisha ulinzi wa vifaa vyao.

"Serikali inatoa fedha nyingi katika kusogeza huduma ya nishati kwa wananchi, baadhi yao wanaihujumu kwa kuiba nyaya za kopa na mafuta kwenye transfoma ambayo zinasaidia kulinda uhai wa transfoma na kufanya kazi vyema, na wanaenda kuuza kama chuma chakavu," anasema Songwe.

Kwa mujibu wa Songwe, matukio ya wizi wa vyuma katika njia za usafirishaji umeme, yamepungua kwa kiasi kikubwa shida ipo katika wizi wa mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma.

**MENEJA SHINYANGA**

Mhandisi Grace Ntungi, ni Meneja wa Tanesco mkoa wa Shinyanga, anataja wizi wa vifaa hivyo, upo zaidi katika kata za Kagongwa Manispaa ya Kahama, na kata ya Bulyanhulu, katika Halmashauri ya Msalala, hata kuchangia umeme kukatika huko kila mara.

Anasema, mpaka sasa zaidi ya transfoma 40 zimeshaharibiwa kwa kuibwa mafuta na nyaya za kopa zinazolinda uhai wake kufanya kazi. Hapo anaomba msaada mkubwa wa Sungusungu, kudhibiti wizi huo.

Meneja huyo wa Tanesco ana maoni kwamba Sungusungu wahakikishe kuwa mstari wa mbele, kuhakikisha wanatokomeza vitendo hivyo, kwa sababu wahujumu wanaishi yao mtaani, ikiwezekana kukomesha tabia hiyo.

Katika hilo, Festo Kiswaga, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anawataka sungusungu wote kufanya mikutano katika maeneo yao kuwaleza wananchi haja ya kulinda miundombinu ya umeme.

Hapo inatangazwa, sungusungu atakayemkamata mwizi anayehujumu atapewa zawadi Sh.500, 000 na cheti cha ushujaa, akifafanua lengo kuinufaisha Tanesco, wananchi, pia serikali.

Mkuu wa Wilaya anatoa tahadhari kwamba, itaanza kuwachukulia hatua kwanza makamanda wa Sungusungu, kwani wao ndio wanaishi na wanajamii.

"Mkimkuta mwizi akiwa anahujumu miundombinu ya shirika hakikisheni mnamuwajibisha kisheria na kutoa taarifa kituo cha polisi kwa hatua zaidi za kisheria na mkimkuta amefika kwenye transfoma baada ya kutokea kwa shoti, toeni taarifa Tanesco," anasema Kiswaga.

Anaendelea:"Hawana akili wote wanaohujumu miundombinu, kwa sababu wanaiba vitu vya gharama kubwa na kwenda kuuza kama chuma chakavu tena kwa fedha kidogo,na kwa mara ya mwisho wezi hao waliiba Transfoma ya Kata ya Kagongwa".

Mwenyekiti wa Sungusungu Wilaya, Muzari Kashindya, anaahidi watahakikisha wanafanya mikutano ya kila mara kukumbushana wajibu wa jeshi lake la jadi, ikiwemo kulinda miundombinu ya Tanesco na anaomba Polisi kuwapa ushirikiano.

Anakiri ni zaidi ya miaka mitatu hawajafanya mikutano ya kukumbushana majukumu yao na wengi walijisahau kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao, hata kuchangia kuibuka wizi wa namna hiyo.

Sungusungu Paul Mabula na Samwel Mpengo, wanaahidi kuingia katika mapambano na watashirikiana na wananchi kuibua wahalifu walioko.

Mpengo anaisihi Tanesco, kuhakikisha wanapopeleka nyaya vijijini kuwafungia huduma wananchi, wawe wanawajulisha zilizosalia ili wao Sungusungu, wahakikishe wanazilinda.

Pia, Mpengo analiomba shirika kuwapatia orodha kamili ya transfoma zilizopo katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama, ili waelekeze nguvu za ulinzi huko.

UKURASA 11

# Nipashe

Ijumaa Julai 29, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581021
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Uteuzi ma-RC, ma-RAS waibua gumzo

UKURASA 2





Dk. Binilifu Satano Mahenge


Joseph Mkirikiti


Meja Jenerali Charles Mbuge


Mhandisi Robert Gabriel


Ally Hapi


Brigedia Jenerali Marco Gaguti


Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge


David Kafulila


Stephen Kagaigai

## NDANI


Albert Chalamila
**Kagera**


Dk. Raphael Chegeni
**Mara**


Fatma Mwasa
**Morogoro**


Halima Dendego
**Iringa**


Peter Serukamba
**Singida**

# Kinana amshauri IGP kero askari usalama barabarani

UKURASA 2

## Ndalichako azishukia h'shauri mafao ya wastaafu

UKURASA 3



**MICHEZO** HATIMAYE MUGALU, KAGERE YAMETIMIA UK.24
**MAONI, KATUNI** UK.6

## Kinana amshauri IGP kero askari usalama barabarani

**Beatrice Shayo na Maulid Mmbaga,** SONGWE

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali mstaafu Abdulrahman Kinana, amemshauri Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camilius Wambura, kuangalia kufanya tathmini ya wingi wa askari wa usalama barabarani maeneo ya mijini.

Amesema wingi wa askari hao umesababisha kero na malalamiko kutoka kwa wananchi. Kinana alitoa ushauri huo jana kutokana na malalamiko aliyopokea kutoka kwa wananchi mbalimbali wakiwamo madereva, waliomweleza uwapo wa utitiri wa askari hao na kuomba chama kuingilia kati.

Malalamiko hayo pia yalijitokeza kwenye kikao cha wanachama wa CCM kilichofanyika mkoani hapo wakati wa ziara ya Kinana ambaye ameambatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, wakikagua miradi ya maendeleo na utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama.

Mmoja wa wananchi hao, Joseph Mwakifule, alisema kutoka Mbozi hadi Tunduma kumekuwa na askari wengi licha ya kuwa na vituo 15 na kujikuta wanatoa fedha kuanzia Sh. 2,000 hadi Sh. 5,000. Kutokana na malalamiko hayo, Kinana alisema, kwanza, anampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua IGP mpya na ana hakika kiongozi huyo wa polisi ni mwadilifu, hodari na ni mchapa kazi.

Kinana alisema anamwomba IGP na vyombo vyake kutazama utaratibu mzima wa askari wa usalama barabarani kuwa wengi maeneo ya mijini.

Unaondoka unaenda hatua moja unasimamishwa, mara unaambiwa washa taa. Sasa niwashe taa ya nini mchana? Nataka nimsihi IGP afanye tathmini juu ya hali ya trafiki wengi walioko kwenye miji yetu," alisema Kinana huku akiweka bayana kuwa hali hiyo imekuwa kero kwa watu.

Alisema biashara nyingi zinaharibika, kuchelewa kutokana na kila wakati kuambiwa upaki pembeni. Watu wanakerwa na kusimamishwa mara kwa mara.

Nipashe ilizungumza na Selemani Omari, dereva wa lori linalofanya safari kutoka Dar es Salaam kwenda Mbeya na kuthibitisha kukutana na usumbufu mkubwa barabarani kutokana na trafiki kuwasimamisha mara kwa mara huku akishauri uwekwe utaratibu maalumu wa ukaguzi.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (katikati), akiwa kwenye Mkutano Mkuu wa 41 wa Taasisi ya Shelter Afrique katika mji wa Victoria Falls, nchini Zimbabwe jana. **PICHA: WANMM**

# Uteuzi Ma-RC, Ma-RAS wazua gumzo

**Na Waandishi Wetu**

UTEUZI wa viongozi wa ngazi za mikoa, hususan wakuu wa mikoa uliofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan jana, umezua gumzo kutokana na baadhi kung'ara tena akiwamo, Albert Chalamila ambaye amerejea kwa mara nyingine.

Rais Samia alifanya mabadiliko ya wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa huku wengine wakiondolewa kwenye nyadhifa hizo na katika wakuu wa mikoa, wanawake watano walichomoza hivyo kufanya idadi yao kuwa wanane sawa na asilimia 30.76.

Kutokana na uteuzi huo, watu walitoa maoni yao kupitia mitandao ya Twitter, Instagram na Facebook, wengi wakipongeza wakisema unalenga kuimarisha safu ya utendaji kazi wa Rais Samia.

Mmoja ya watu walioandika maoni kwenye ukurasa wa twitter wa Ikulu Mawasiliano, aliandika: "Mlimtumbua Chalamila kwa nini na mmemrudisha kwa sababu zipi?" huku Mwinyi Salim akiandika: "Chalamila karudi kazini leo Ally Hapi kibarua kimeota nyasi."

Naye Augustino Amando aliandika: "(Anthony) Mtaka alistahili kwenda Dar es Salaam na si Njombe, nimefurahi kuona Ally Hapi kaondolewa lakini sijafurahi Chalamila kurudi tena."

Nicolaus Luhwago alisema: "Hii inatufundisha nini Watanzania? Ukitenguliwa kaa kimya wala kutoongea maneno mabaya, hongera sana Chalamila." Huku Millanzi Marry akisema: "Viboko Kagera vitawahusu wale wazembe."

Camel aliandika: "Wakati umefika wa kuangalia weledi katika kuwapa watu madaraka. Tujenge nchi hii kwa uchungu na maarifa makubwa, tujitahidi kuacha alama hasa kwenye kuwasaidia wananchi. Tumalize umasikini, ujinga na maradhi, tusiweke siasa linapokuja suala la utendaji serikalini, tuwe wasikivu kidogo."

Kwa takribani siku 412 tangu atenguliwe akiwa mkuu wa mkoa wa Mwanza, Chalamila alikuwa akionekana kwenye mitandao ya kijamii akitoa mahubiri na kuimba nyimbo mbalimbali.

Miongoni mwa nyimbo hizo ni wa 'Galilaya Yesu alitembea juu ya maji kwa uweza wa Mungu'. Picha nyingine ya video alionekana akiimba 'Tukimaliza kazi tutavalishwa taji'.

Kauli yake ya kuwataka wananchi kujitokeza na mabango hata yenye matusi katika ziara ya Rais Samia mkoani Mwanza, ilidaiwa kuwa sababu za kutumbuliwa kwake. Kauli hiyo ya Chalamila ilikuja siku chache baada ya Rais Samia kuonya tabia za ulipukaji kwa viongozi aliowateua.

**MAONI YA WACHAMBUZI**

Baadhi ya wachambuzi walitoa maoni yao akiwamo Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Paul Loisulie, aliyesema walioteuliwa wameaminika kuleta hali mpya kwenye serikali.

"Waliobakizwa kwenye mikoa bado wana nafasi ya kufanya vizuri zaidi kwa kuwa wamemudu. Walioachwa huenda viatu vimewabana, kwa kuwa jukumu walilopewa huenda hawatimizi wajibu wao kama inavyotarajiwa na Rais na wananchi," alisema.

Kuhusu Chalamila, alisema: "Chalamila aliondolewa kwenye nafasi na amerudishwa. Kwa wakati ule ilionekana apumzike lakini kwa sasa ameonekana anafaa kurudi. Kwa ujumla, uteuzi huu unatafsiri mbalimbali lakini lengo ni kupata watu ambao watamsaidia kutekeleza ahadi kwa wananchi."

Naye mchambuzi wa siasa, uchumi na jamii, Jawadu Mohamed, alisema Rais anapanga serikali yake vizuri ili kuleta matokeo chanya kwa wananchi.

**JINSIA YAZINGATIWA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, alipongeza uteuzi uliofanywa na Rais Samia kwa kile alichosema ametekeleza kwa vitendo kile alichoahidi hasa kuongeza idadi ya wanawake.

"Katika nafasi hizi alizozitoa kwa wakuu wa mikoa, tunamshukuru kwa sababu wanawake wameongezeka japo kidogo. Tunachosisitiza, tunatamani vitu vya kudumu na endelevu vifanyike," alisema.

Mchambuzi wa siasa , Gwandumi Mwakatobe, ambaye pia ni muumini wa harakati za kijinsia, alisema wanapozungumzia usawa wa kijinsia, hawazungumzii namba, bali mtu yeyote apewe nafasi kulingana na weledi, sifa na uwezo alio nao na si jinsi.

"Asiteuliwe mtu kwa sababu ni mwanamke. Ateuliwe kwa sababu ana uwezo kuwazidi wengine. Tuangalie anayefanya kazi pale ni kwa sababu ana sifa na uwezo wa kuleta matokeo mazuri na si kwa sababu ni mwanamke au mwanamume. Vigezo vya maumbile visitumike kitumike kigezo cha weledi, sifa na uwezo alionao mtu," alisisitiza.

**UTEUZI USIKU WA MANANE**

Alfajiri ya jana, Rais Samia alifanya uteuzi wa wakuu hao pamoja na makatibu tawala wa mikoa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, Rais Samia amefanya uteuzi huo wa watu wapya, kuwahamisha vituo vya kazi huku wengine wakitemwa.

**WALIOTEMWA**

Wakuu wa Mikoa waliotemwa ni Stephen Kigaigai (Kilimanjaro), David Kafulila (Simiyu), Robert Gabriel (Mwanza), Ally Hapi (Mara), Brigedia Jenerali Marko Gaguti (Mtwara), Brigedia Jenerali Wilbert Ibuge (Ruvuma), Meja Jenerali Charles Mbuge (Kagera), Dk. Binilith Mahenge (Singida) na Joseph Mkirikiti (Rukwa).

Kwa upande wa Makatibu Tawala wa Mikoa miongoni mwa walioachwa ni Prof.Faustine Kamuzora(Kagera),

**WALIONG'ARA**

Walioteuliwa ambao waliwahi kushika nafasi hizo na wamerejea baada ya kukaa benchi kwa miaka kadhaa na mikoa mipya kwenye mabano ni Fatma Mwasa (Morogoro) na Halima Dendego (Iringa).

Wengine waliong'ara na mikoa kwenye mabano ni Nurdin Babu (Kilimanjaro), Dk. Raphael Chegeni (Mara), Peter Serukamba (Singida), Kanali Ahmed Abbas Ahmed (Mtwara), Kanali Laban Thomas (Ruvuma) na Dk. Yahaya Nawanda (Simiyu)

Kanali Ahmed, Kanali Thomas, Nurdin Babu, na Dk. Nawanda kabla ya uteuzi huo walikuwa wakuu wa wilaya za Kibiti, Nyasa, Longido na Tabora.

Kwa upande wa Ma-RAS, Kamishna Dk.Mussa Ali Mussa (Morogoro), Prof. Godius Kahyarara (Geita), Alikuwa Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mhandisi Leonard Masanja (Iringa), alikuwa Mkufunzi wa Chuo cha Tanesco mkoani Dar es Salaam, Toba Nguvila (Kagera) alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Elikana Balandya (Mwanza), alikuwa Kamishna wa Bajeti Wizara ya Fedha na Mipango, Prof. Siza Tumbo (Shinyanga), alikuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo na Dk. John Mboya (Tabora), alikuwa Kamishina wa Idara ya Bajeti katika Wizara ya Fedha na Mipango.

**WALIOHAMISHWA VITUO**

Katika uteuzi huo, aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma Anthony Mtaka amehamishiwa Njombe, Queen Sendiga amehamishiwa Rukwa akitokea Iringa, Waziri Kindamba amekwenda Songwe kutoka Njombe, Martine Shigella amepelekwa Geita akitokea Morogoro.

Wengine ni Omary Mgumba kutoka Songwe kwenda Tanga, Adam Malima (Tanga kwenda Mwanza) huku Rosemary Senyamule akihamishiwa Dodoma kutoka Geita.

Kwa upande wa Ma-RAS, Missaile Musa amekwenda Arusha akitokea Songwe, Rehema Madenge amehamia Dar es Salaam kutoka Lindi, Hassan Rugwa (Dar es Salaam kwenda Katavi), Ngusa Samike (Lindi kutoka Mwanza).

Wengine ni Msalika Makungu (Mara kutoka Tabora), Albert Msovela (Mara kwenda Kigoma), Rodrick Mpogolo (Katavi kwenda Mbeya), Zuwena Jiri (Pwani kutoka Shinyanga) Happiness Seneda (Iringa kwenda Songwe) na Rashid Mchata (Kigoma kwenda Rukwa).

**WALIOBAKI VITUONI**

Wakuu wa mikoa waliobaki vituoni ni Amos Makala (Dar es Salaam), John Mongella (Arusha), Mwanamvua Mrindoko (Katavi), Makongoro Nyerere (Manyara), Zainab Telack (Lindi), Juma Homera (Mbeya), Thobias Andengenye (Kigoma), Sophia Mjema (Shinyanga), Balozi Batilda Burian (Tabora) na Abubakar Kunenge (Pwani).

Ma-RAS waliobaki ni Dk. Fatuma Mganga (Dodoma), Karolina Mthapula (Manyara), Abdallah Malela (Mtwara), Judica Omary (Njombe), Willy Machumu (Kilimanjaro), Steven Ndaki (Ruvuma), Dorothy Mwaluko (Singida), Prisca Kayombo (Simiyu) na Pili Mnyema (Tanga).

■**Imeandaliwa na Augusta Njoji (DODOMA), Romana Mallya (Dar), Thobias Mwanakatwe (Singida).**

HABARI KITAIFA

# Ndalichako aziwakia h'shauri kuchelewesha mafao wastaafu

**Na Richard Makore,** MWANZA

SERIKALI 'imeziwashia moto' halmashauri mbalimbali kwa kushindwa kuwasilisha michango ya wafanyakazi wao na kusababisha wastaafu kutolipwa mafao yao kwa wakati huku wengine wakisota kwa zaidi ya miaka minne.

Akizungumza na wastaafu jijini Mwanza jana kutoka Mkoa wa Mwanza na mikoa jirani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, Profesa Joyce Ndalichako, alisema chanzo cha waliokuwa watumishi hao kuchelewa kupata mafao yao ni kutokana na kukosekana michango yao katika mifuko ya jamii.

Alisema wastaafu wengi wanapata shida kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo halmashauri na sekta binafsi kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye mifuko ya jamii.

Profesa Ndalichako alisema halmashauri zote zinatakiwa kuwasilisha michango ya watumishi wao kwa kuwa hilo ni takwa la kisheria.

"Nazitaka hizi halmashauri kuhakikisha zinawasilisha michango ya watumishi wake kwa wakati ili kuwasaidia wanapostaafu waweze kulipwa mafao yao," alisema.

"Waajiri wote wasimamie sheria bila shuruti kwa sababu sheria iko wazi mfanyakazi anakatwa asilimia kumi na mwajiri anaongeza asilimia kumi inapatikana asilimia 20 ambayo itawasilishwa kwenye mifuko," alisema.

Aidha, Waziri Ndalichako aliwaomba watumishi wote wa Sekta binafsi na Umma kuwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina mifumo ambayo inawawezesha kufuatilia michango popote walipo kwa kutumia mifumo ya TEHAMA na kupitia simu ya kiganjani mtumishi anaweza kuona taarifa zake mbalimbali.

Alisema kwa upande wa watumishi wa umma serikali imeona tatizo la baadhi ya waajiri hasa wa halmashauri kutowasilisha michango na kwamba kuanzia mwezi Julai mwaka huu, serikali ilichukua ya kukata moja kwa moja michango ya watumishi.

Licha ya kuzimulika halmashauri, Profesa Ndalichako pia alisema sekta binafsi zinachelewesha kuwasilisha michango ya wafanyakazi wake katika mifuko ya PSSF na NSSF jambo ambalo linasababisha usumbufu kwa wastaafu kulipwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Mwanza wakati akizikiliza kero za wastaafu hao ambao walikutana naye ili awasikilize, Profesa Ndalichako alisema kuna watu wamefuatilia mafao yao tangu mwaka 2018 mpaka leo hawajalipwa.

Aliongeza kuwa malalamiko mengine ya wastaafu hao ni pamoja kupunjwa mafao yao na mtumishi anayestaafu kulipwa kidogo ikilinganishwa na mshahara wa mwisho aliokuwa akiupata kabla ya kustaafu.

Alifafanua kuwa jana alipata nafasi ya kuwasikiliza kwa kina wastaafu hao na kwamba shida ambazo zinahusu wizara yake atahakikisha anazitatua.

Profesa Ndalichako alisema kama hali itaendelea kuwa hivi kuna haja ya kubadilisha sheria ili kuwabana waajiri ili kuhakikisha mtumishi anapostaafu kazi analipwa mafao yake.

Kuhusu watumishi wanaolipwa mafao yao na hazina, Profesa Ndalichako alisema wizara yake haihusiki nao na kwamba wale wanaomhusu atahakikisha kila mstaafu analipwa mafao yake na michango inawasilishwa kwenye mifuko kwa wakati.

Mmoja wa wastaafu waliokutana na Waziri Ndalichako, Haindo Ngowi, alisema wastaafu wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo ucheleweshaji wa mafao. Alisema shida zingine wanazokutana nazo ni pamoja na kupunjwa mafao yao huku akisema suala lao linatakiwa kufanyiwa kazi badala ya kusubiri mpaka waziri akutane nao.

Naye mstaafu Benjamin Makabala, aliomba serikali kushughulikia mapema matatizo yao kupitia mifuko yao na sio kusubiri mpaka serikali kutangaza muda wa kuwasaidia.

Aidha, Zaina Mussa alisema kuwa ana imani tatizo lake litashughulikiwa ipasavyo baada ya kikao hicho na waziri na kuwaomba waliopewa dhamana ya kushughulikia matatizo yao wafanye hivyo mapema ili kuleta furaha na kuwaondolea maumivu waliyokuwa nayo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako (wa pili kushoto), akizungumza na baadhi ya wastaafu katika mkoa wa Mwanza na mikoa jirani, alipokutana nao jana, ili kusikiliza kero zao, zikiwamo za kupunjwa, kucheleweshewa mafao na kulipwa mafao yao tofauti na mishahara waliyokuwa wakipata wakati wakiwa kazini. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

# Rais Samia aipaisha Tanzania kimataifa

**Na Jenifer Gilla**

UHUSIANO mzuri wa kidiplomasia baina ya Tanzania na nchi nyingine ulioimarishwa na Rais Samia Suhuhu Hassan, unaelezwa kuipaisha nchi katika nyanja mbalimbali.

Hayo yalisemwa juzi na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula juzi, jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza kuhusu dhana ya diplomasia na utangamano wa kikanda.

Alisema nyanja za kimkakati ni pamoja na afya, kiuchumi na biashara na kwamba wizara inapopanga ziara za Rais ni lazima kuonyesha ushawishi mkubwa kuwa nchi itanufaika na kitu gani kulingana na mikakati ya nchi.

"Yeye kila ziara aliyokuwa anakwenda ilikuwa lazima iwe na ushawishi mkubwa kwamba tunakwenda kupata nini? Ndiyo maana ziara zake ni za tofauti. Kila ziara aliyokwenda ilikuwa kubwa zaidi ni diplomasia ya uchumi, lakini biashara, anafuatana na wafanyabiashara, wawekezaji, lakini pia tumeona tunasaini mikataba mbalimbali katika maeneo ya kimkakati.

"Lakini nashukuru kwamba katika kipindi cha mwaka mmoja tumeona amefungua nchi, tumeimarisha uhusiano baina ya Tanzania na nchi nyingine, jumuiya ya kimataifa kama wanavyosema Tanzania is Back (Tanzania imerudi)," alibainisha Mulamula.

Mulamula aliongeza kuwa uimarishwaji wa diplomasia umeisaidia nchi kupata vifaa vya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 ambao uliiathiri nchi hiyo, ikiwamo msaada wa chanjo hali iliyosaidia nguvu kazi ya taifa kutoathirika sana na kuimarisha uchumi haraka.

"Kabla ya hili janga uchumi wa nchi ulikuwa unakuwa kwa asilimia saba, katika kipindi cha miaka miwili ukaporomoka ikafika asilimia nne, huwezi kusema tunajitosheleza. Kwa hiyo sasa, ndiyo akatoka na kila ziara aliyokwenda lengo lake ni hilo kurudisha uchumi, kuimarisha miundombinu lakini kuwa na miradi ya kimkakati," alisema. Kuhusu Royal Tour, Balozi Mulamula alisema, tangu kufanyika kwa ufunguzi huo Aprili, mwaka huu, nchini Marekani sasa wanapokea wageni wengi kiasi cha mashine zinazotoa viza kwa wageni kuzidiwa.

"Maana yake tumezoea pengine kupokea wageni 10, 20 sasa zinakuja viza 600, mashine zenyewe walivyozitengeneza nadhani hawakutegemea kwamba itatokea kuwe na watu wengi...kwa hiyo tuna wageni wa kila aina," alisema.

Aliwasihi Watanzania kutumia fursa hiyo kuwekeza katika nyanja mbalimbali za biashara ili kuwe na wauzaji wa nje wengi kwa kuwa hadi sasa takwimu zinaonyesha kuwa nchi hiyo inanunua zaidi kutoka nje kuliko kuuza na kuwa serikali inawaunga mkono kwa kujikita zaidi kwenye uzalishaji.

# Mwanafunzi aliyeozeshwa adaiwa kuambukizwa VVU

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWANAFUNZI ambaye jina lake limehifadhiwa, amedaiwa kuambukizwa virusi vya Ukimwi baada ya kuozeshwa ndoa ya utotoni.

Mwanafunzi huyo, imeelezwa aliogeshwa dawa ya mvuto wa mapenzi, maarufu kama samba na wazazi wake ili apate mume wa kumwoa kwa lengo la wao kupata mifugo.

Mratibu wa Miradi kutoka Shirika la Rafiki-Sdo mkoani Shinyanga, Mariam Maduhu, alibainisha hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya tathmini ya ufungaji wa mradi wa kupinga matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani hapo.

Alisema wakati wa utekelezaji wa mradi huo, wamekumbana na matatizo ya wazazi kwenye Kata ya Ilola, kuwaogesha watoto wao wa kike dawa ya mvuto wa mapenzi, ili wapate wanaume wa kuwaoa na kupata utajiri wa mifugo.

"Wakati wa utekelezaji wa mradi, tumekumbana na mwanafunzi ambaye aliogeshwa 'samba' akaolewa na kuacha masomo. Lakini hakudumu kwenye ndoa yake akaachika huku tayari akiwa ameshaambukizwa virusi vya Ukimwi," alisema Maduhu.

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii wilayani Shinyanga, Deus Mhoja, alisema jamii bado inapaswa kuendelea kupewa elimu juu ya ukatili hasa kwa watoto ambao ndio waathirika wakubwa na hata kuzima ndoto zao.

Alisema matukio ya ukatili dhidi ya watoto na wanawake wilayani hapo bado yapo lakini yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na wadau mbalimbali kuendelea kutoa elimu pamoja na wahusika kuchukuliwa hatua, wakiwamo wazazi na wahusika wa ndoa na ukatili.

Pia alisema serikali katika mwaka wa fedha (2022/23 katika Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri hiyo, imetengewa Sh. milioni 20 kwa ajili ya mapambano dhidi ya ukatili kwa watoto na wanawake.

Naye Mratibu wa Mfuko wa Ruzuku wa Wanawake Tanzania (WFT-Trust) mkoani Shinyanga, Glory Mbia, ambao wametoa ufadhili wa fedha kwa wadau kutekeleza mradi wa kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto wilayani Shinyanga, alisema licha ya mradi huo kuisha, serikali inapaswa kuendeleza mapambano na kumaliza kabisa ukatili ndani ya jamii.




Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Dk. Respcious Boniface, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kuhusu mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za taasisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wagonjwa majeruhi ajali barabarani waongoza

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Tiba ya Mifupa Muhimbili (MOI), Dk. Respicious Boniface, amesema majeruhi wa ajali za barabarani wanaongoza kwa idadi kubwa ya wagonjwa wanaopokelewa na taasisi hiyo.

Pia ametaja sababu ya ndugu kuwatelekeza wagonjwa hao kuwa ni kushindwa kulipa gharama za matibabu, kwa mgonjwa aliyevunjika mguu au kichwa matibabu yake ni kuanzia Sh. milioni 1.5 hadi Sh. milioni 30, kulingana na muda wa kukaa wodini.

Mkurugenzi huyo alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za taasisi hiyo kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Alisema majeruhi wengi ni wa ajali za pikipiki (bodaboda) pamoja na magari na kuiwataka Watanzania kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kupunguzia mzigo serikali wa kuhudumia majeruhi hao.

Hata hivyo, alikanusha uvumi unaosambaa katika maeneo mbalimbali nchini kuwa majeruhi wa bodaboda wanakatwa miguu wanapofikishwa katika taasisi hiyo. "Sisi mafunzo yetu yanatutaka kwanza kuangalia namna ya kuokoa kiungo badala ya kukikata hata kama mfupa umevunjika mara nyingi, tunatakiwa kutoa uangalizi wa saa 12 baada ya hapo kama utakuwa unaweza kuleta madhara katika jeraha lile ndipo tunapaswa kukata," alisisitiza Dk. Boniface.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 4.2 kwa ajili ya ununuzi wa 'Implants' (viungo) ili kukabiliana na changamoto ya uhaba kwa wagonjwa.

"Vifaa hivi vimesaidia kuendelea kuboresha huduma za matibabu ya kibingwa ya mifupa, ubongo, uti wa mgongo na mishipa ya fahamu, hivyo kuokoa maisha ya Watanzania wengi na pesa za serikali ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu," alisema Dk. Boniface.

Pia alisema katika kipindi cha mwaka mmoja jumla ya wagonjwa 7,113 walifanyiwa upasuaji ikilinganishwa na wagonjwa 6,793 waliofanyiwa katika mwaka uliopita wa 2020/2021 ikiwa ni ongezeko la asilimia mbili.

"Upasuaji mbalimbali wa kibingwa uliofanyika ni pamoja na kubadilisha nyonga 207, kubadilisha magoti 182 upasuaji wa mfupa wa kiuno 96, wagonjwa 200 wamefanyiwa upasuaji wa magoti na mabega kwa njia ya matundu kati yao waliofanyiwa mabega ni 32 na magoti ni 168, wagonjwa 249 wamefanyiwa upasuaji wa uti wa mgongo kwa kufungua eneo dogo (minimal invasive spine surgery)," alisema.

Kadhalika, katika kipindi cha mwaka mmoja watoto 17 wamefanyiwa upasuaji wa kunyoosha vibiongo (scoliosis), wagonjwa 11 wamefanyiwa upasuaji wa kuondoa vivimbe vya mishipa ya damu kwenye ubongo (cerebral aneurysm repair).

"Gharama za matibabu haya ndani ya nchi zilikuwa Sh. bilioni 10.2 na kama wangepelekwa nje ya nchi kwa matibabu jumla ya Sh. bilioni 42.7 zingetumika. Hivyo taasisi imeokoa Sh. bilioni 32.5, ambazo zitatumika kwa huduma nyingine za maendeleo ya nchi," alisema.

Alizitaja huduma mpya zilizoanzishwa na aassi hiyo katika kipindi hicho kuwa ni huduma ya kuondoa uvimbe kwenye sakafu ya ubongo kupitia tundu la pua na wagonjwa 19 wameshafanyiwa upasuaji.

"Gharama za upasuaji huu hapa nchini ni Shilingi milioni nane na nje ya nchi ni Sh. milioni 40, hivyo Taasisi imeokoa zaidi ya Sh. 608,000,000 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa hawa nje ya nchi," alisema. Alisema huduma nyingine ni matumizi ya maabara ya upasuaji wa ubongo na katika kipindi hiki wagonjwa 186 wamehudumiwa.

Alisema gharama za huduma hiyo nchini ni kati ya Shilingi milioni tano hadi 10 na nje ya nchi ni Sh. million 30 hadi 60, Taasisi imeokoa kati ya Sh. bilioni 5.6 hadi Sh. bilioni 11.2 ambazo zingetumika kupeleka wagonjwa hawa nje ya nchi.

"Huduma hizi mpya, zimeiwezesha taasisi kupunguza kwa kiasi kikubwa rufaa za wagonjwa nje ya nchi. Ambapo kwa sasa kwa magonjwa ya Neurosurgeries asilimia 96 tunafanya hapa na upasuaji wa mifupa asilimia 98 tunafanya hapa," alisema.

# TEF yaeleza umuhimu mabadiliko sheria za habari

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile, amesema mchakato wa mabadiliko ya sheria za habari ni kupata uhuru wa kihabari na kuondoa sheria zinazovizia wanahabari ili kuwaingiza matatani.

Akizungumza katika Kipindi cha 360 kinachorushwa na Kituo kimoja cha Luninga jana jijini Dar es Salaam, alisema mchakato huo unalenga pia kuweka mipaka na na malengo ya uhuru wa habari bila kuumiza wengine.

"Mchakato wa mabadiliko haya, unalenga kuweka mipaka lakini pia uhuru wa habari bila kuumiza mtu yeyote. Tunalenga kupata uhuru zaidi wa habari na wajibu kwa mwanahabari.

"Tunapozungumzia uhuru wa vyombo vya habari, sio kwamba tunataka upendeleo kutoka serikalini, Tunacholenga hapa kila mmoja apate haki na awajibike," alisema Balile.

Kadhalika, alisema ingawa wadau wa habari wanasimamia mabadiliko hayo, uhuru wa habari unawahusu hata wale wasio wanahabari.

"Kwamba, nchi ambayo uhuru wa habari haupo, wananchi hukosa fursa ya kupata taarifa sahihi na hivyo kunyima haki yao ya msingi ya kuhabarika.

"Tufahamu kuwa uhuru wa habari ni haki ya msingi ambayo wengine wanaitaka. Vyombo vya habari visipokuwa huru, wananchi nao pia wanakosa uhuru ikiwa ni pamoja na kutoa maoni yao pia kupata taarifa zinazowahusu moja kwa moja," alifafanua Balile.

Alitoa mfano wa ajali iliyotokea Mtwara na kusababisha vifo vya wanafunzi wanane kwamba, watu wamefahamu nini kimeendelea kutokana na ajali hiyo, lakini uhuru wa kutoa habari bado haujalindwa kisheria, "Ndio maana tunataka hapa ulindwe na sheria."

Alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kupitia sheria za habari na kuagiza zifanyiwe maboresho ili kuendana na mazingira yaliyopo.

"Tulikutana na Rais Samia Ikulu na kwa kuanza, tulimuomba kuhamisha tasnia ya habari na kuipeleka kwenye Wizara ya Mawasiliano, tunashukuru amefanya hivyo.

"Tukasema sasa tutengeneze muwngiliano mzuri wa sheria, na jambo zuri ni mchakato umeanza, lakini siku za karibuni hapa, umepoa," alisema.

Alimkumbusha Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, kuongeza kasi ili kufikia matamanio ya wadau wa Tasnia ya Habari.

# Serikali za mitaa kinara rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI za Mitaa zimetajwa kuongoza kwa vitendo vya rushwa katika utendaji kazi wao, kwenye taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapa, Sosthenes Kibwengo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kibwengo alisema eneo linaloshika nafasi ya pili ni Elimu, ikifuatiwa na Polisi, huku upande wa Manunuzi na Ardhi.

Akitaja taasisi hizo na asilimia zake kwenye mabano ni Serikali za Mitaa (15), Elimu (11), Polisi (10), Manunuzi (6) na Ardhi (5).

Kibwengo, alisema kwa upande wa sekta binafsi, Misitu, Fedha na Afya kila mmoja wana asilimia nne huku Maji wakiwa na asilimia tatu na sekta nyingine zina asilimia tano.

Alisema taasisi hiyo imefuatilia miradi 77 ya maendeleo yenye thamani ya Sh. million 19.5 ambayo ni katika sekta ya maji, afya, elimu na ujenzi na kwamba kati ya hiyo miradi 58 yenye thamani ya Sh. million 10.4 ilitekelezwa kwa fedha za UVIKO-19.

Hata hivyo, alisema wataendelea na ufuatiliaji ikiwamo kutoa elimu kwa jamii ili kuhakikisha kila mmoja anashiriki katika mapambano dhidi ya rushwa ili kusaidia jitihada za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa.

Alifafanua kuwa, pia taasisi hiyo mkoani Dodoma imefanikiwa kuokoa Sh. milioni 10.9 huku akisema watendaji 17 waliofuja mali za jumla ya Sh. million 179.3 wamechunguzwa na tayari mashauri 15 ya ubadhilifu yameshafikishwa mahakamani.

"Takukuru inaendelea na jitihada za utoaji elimu kwa jamii ili kuhakikisha rushwa inatokomezwa," alisema Kibwengo.

Alisema taasisi hiyo mkoani hapa imefanikiwa kukusanya taarifa 111, kati ya hizo 71 zilihusu masuala ya rushwa huku 40 zikiwa hazihusiani na rushwa.

Akizungumzia mikakati waliyopanga ili kuhakikisha wanatokomeza rushwa katika maeneo mbalimbali, Kibwengo alisema, wamefungua milango kwa wananchi kutoa taarifa endapo wataona mahali kuna ubadhirifu unafanywa, ikiwamo kutoa taarifa ambazo zina viashiria vya rushwa.

Katika sekta ambazo zimeonekana kuwa sugu katika asilimia za uwepo wa vitendo vya rushwa wataendelea kuzifanyia kazi, pia amewataka wananchi kutoa ushirikiano ili kuhakikisha wanafikia malengo waliojiwekea kwenye mapambano dhidi ya rushwa.

Aliwataka watumishi na wananchi kubadili mtazamo wa utendaji kazi wao ili kuhakikisha wanakuwa mabalozi katika maeneo ambayo wanaendesha shughuli zao za utendaji kazi zao za kila siku.

Akizungumzia masuala ya utoaji elimu katika maeneo mbalimbali, Kibwengo alisema wanaklabu za wapinga rushwa katika shule za msingi, sekondari pamoja na vyuo ambazo zilitembelewa na kuelimishwa kuhusua madhara ya rushwa ikiwamo kuziimarisha.

Kibwengo alisema lengo la kuwa na klabu katika shule na vyuo ni pamoja na kutaka wanafunzi hao wanapohitimu wakawe mabalozi katika maeneo mbalimbali wanayoishi.

TANGAZO

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## Tanzu ya Citigroup, Kampuni iliyoshirikishwa nchini Marekani

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 31-Mac-22 |
|---|---|---|
| **A . MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 15,496 | 11,981 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 63,908 | 132,126 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 197,778 | 196,643 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 394,996 | 245,009 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 140 | 290 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | 23,517 | 15,619 |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 29,149 | 21,445 |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 100,275 | 48,867 |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 356,717 | 302,201 |
| 12 Mali Nyingine | 15,435 | 12,026 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,951 | 7,090 |
| 16 **JUMLA YA MALI** | **1,204,362** | **993,297** |
| **B . DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 312 | 886 |
| 18 Amana za Wateja | 834,946 | 740,653 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | 9 | 9 |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 2,379 | 2,472 |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,084 | 3,556 |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 29,160 | 21,450 |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine | 712 | 632 |
| 27 Dhima Nyingine | 34,074 | 25,036 |
| 28 Madeni | 198,240 | 93,080 |
| 29 **JUMLA YA DHIMA** | **1,103,915** | **887,774** |
| 30 **MALI/(DHIMA) HALISI** | **100,447** | **105,523** |
| **C . FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 - Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,660 | 9,660 |
| 32 - Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 - Mapato Yaliyobakizwa | 82,441 | 90,005 |
| 34 - Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 6,433 | 3,175 |
| 35 - Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,913 | 2,683 |
| 36 - Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **100,447** | **105,523** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 104,829 | 99,181 |
| 39 Mikopo Chechefu | - | - |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,348 | 884 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| ( i ) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 8.3% | 10.6% |
| ( ii ) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.0% | 0.0% |
| ( iii ) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 42.7% | 40.8% |
| ( iv ) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 29.6% | 30.4% |
| ( v ) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 78.8% | 74.9% |
| ( vi ) Ongezeko la Amana | 11.2% | -24.0% |
| ( vii ) Ongezeko la Mali | 17.5% | -16.0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Jun-22 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 8,477 | 8,395 | 15,827 | 15,215 |
| 2 Gharama za Riba | (1,746) | (2,383) | (3,251) | (4,607) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba** | **6,731** | **6,012** | **12,576** | **10,608** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (464) | (326) | (140) | (233) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **4,891** | **3,238** | **10,248** | **6,620** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 3,458 | 2,005 | 5,624 | 4,113 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,433 | 1,233 | 2,860 | 2,507 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 1,764 | 0 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(6,718)** | **(5,813)** | **(13,529)** | **(11,474)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (3,121) | (2,255) | (6,091) | (4,488) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | (3,596) | (3,559) | (7,438) | (6,986) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **4,440** | **3,111** | **9,155** | **5,522** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (1,182) | (1,092) | (2,723) | (1,732) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **3,258** | **2,019** | **6,433** | **3,790** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | | | |
| Mapato ambayo hayajakamilika | (1,100) | 1,075 | (154) | (82) |
| Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 330 | (323) | 46 | 25 |
| Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | (770) | 753 | (108) | (57) |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa** | **2,488** | **2,772** | **6,325** | **3,733** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 55 | 45 | 55 | 45 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 325,812 | 201,940 | 643,287 | 379,005 |
| 15 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **D . BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| ( i ) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.1% | 0.8% | 1.2% | 0.8% |
| ( ii ) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 13.0% | 8.4% | 12.7% | 7.8% |
| ( iii ) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 57.8% | 62.8% | 59.3% | 66.6% |
| ( iv ) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 4.3% | 3.3% | 4.2% | 2.7% |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Imesainiwa na: Geofrey Mchangila (Ofisa Mtendaji Mkuu) — Date : 28 Julai 2022

Imesainiwa na: Iddi Msonga (Mkuu wa Fedha) — Date : 28 Julai 2022

Imesainiwa na: Godwin Rutashobya (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) — Date : 28 Julai 2022

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

Imesainiwa na: Andulile Mwakalyeye — Date : 28 Julai 2022

Imesainiwa na: Wilson Chola — Date : 28 Julai 2022

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-22 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mac-22 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-22 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka 30-Jun-21 |
|---|---|---|---|---|
| **I . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 4,440 | 4,716 | 9,155 | 5,522 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| -Hasara Katika Mali | 491 | 484 | 975 | 893 |
| -Badiliko Halisi Katika Mikopo | (54,515) | (11,702) | (66,218) | 10,543 |
| -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (0) | 36 | 36 | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana | 93,719 | (177,649) | (83,929) | (431,901) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 8,859 | 14,120 | 22,980 | (5,107) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (18,216) | (10,261) | (28,477) | (2,525) |
| -Kodi Iliyolipwa | (886) | (886) | (1,772) | (1,293) |
| -Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **33,891** | **(181,142)** | **(147,250)** | **(423,868)** |
| **II . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (274) | - | (274) | (52) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | (2,235) | (11,387) | (13,623) | (25,110) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(2,509)** | **(11,387)** | **(13,897)** | **(25,163)** |
| **III . Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 105,160 | 880 | 106,040 | 5,000 |
| Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **105,160**<br>**136,542** | **880**<br>**(191,649)** | **106,040**<br>**(55,107)** | **5,000**<br>**(444,031)** |
| **IV . Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **136,542** | **(191,649)** | **(55,107)** | **(444,031)** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 438,272 | 629,921 | 629,921 | 808,060 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 574,814 | 438,272 | 574,814 | 364,029 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 JUNI 2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | - | **89,400** | **605** | - | **2,021** | **101,686** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 6,433 | - | - | - | **6,433** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (108) | **(108)** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | - | - | (7,564) | - | - | - | **(7,564)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 605 | (605) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | - | **88,874** | - | - | **1,913** | **100,447** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | **9,660** | - | **85,916** | **1,582** | - | **1,759** | **98,917** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 3,790 | - | - | - | **3,790** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (57) | **(57)** |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa/litakalolipwa | - | - | (5,057) | - | - | - | **(5,057)** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 1,266 | (1,266) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **9,660** | - | **85,915** | **316** | - | **1,702** | **97,593** |

## CHARGES AND FEES- CITIBANK TANZANIA LIMITED

**1.0**

| Current Accounts | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | Waived | Waived |
| (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 20,000 | USD $20 |
| (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 4,000 | US$ 5.00 |
| (d) Fees per ATM withdrawal | N/A | N/A |
| (e) ATM mini statement | N/A | N/A |
| (f) Interim statement per page | TZS 7,000 | US$ 5.00 |
| (g) Periodic scheduled statement | Waived | Waived |
| (h) Cheque book | TZS 35,000 (100 leaves) | US$ 35 (100 leaves) |
| (i) Dishonoured cheque | TZS 52,000 | US$ 50 |
| (j) Special clearance | TZS 60,000 | US$ 60 |
| (k) Counter cheque | TZS 2,500 per leaf | US$ 2 per leaf |
| (l) Stop Payment | TZS 30,000 | US$ 30 |
| (m) Standing order | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| (n) Balance enquiry | Waived | Waived |
| (o) New ATM card issuance | N/A | N/A |
| (p) ATM card renewal or replacement | N/A | N/A |
| (q) Overdrawn account interest charge | 4.67%-8.92% | 1.75%-7.78% |
| (r) Unarranged overdraft | 15% | 10% |
| (s) Interbank transfer | Waived | Waived |
| (t) Bill payments through ATM | N/A | N/A |
| (u) Deposit fee | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 | US $20 and below: 3% of deposited amount<br>TZS 1,000 and below: 0.3% of deposited amount<br>Coins: 3% of the deposited amount minimum TZS 10,000 |
| (v) Other (please specify) | N/A | N/A |
| (w) BRELA Search fees. Per search | TZS 30,000 | US$ 15 |
| (x) Foreign Loan Registration fees (DRN) | US$ 700 | US$ 700 |

**2.0 Savings Accounts**

| | | |
|---|---|---|
| (a) Required minimum opening balance | NA | NA |
| (b) Monthly service fee | NA | NA |
| (c) Interim statement | NA | NA |
| (d) Account clossure | NA | NA |

**3.0 Electronic Banking**

| | | |
|---|---|---|
| (a) Internet banking monthly fee | Waived | Waived |
| (b) Internet transfers | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00<br>USD TISS: US $ 10.00 | EFT: TZS 5,000<br>TZS TISS: TZS 10,000<br>Cross Border Fund Transfers: 0.25% of transfer, Min US$ 60.0 and Max US$ 500.00 USD TISS: US $ 10.00 |
| (c) SMS banking | N/A | N/A |
| (d) Other | Managers Cheques: TZS 4,000 | Managers Cheques: US$ 5.00 |

**4.0**

| Foreign Exchange Transactions | CHARGE/FEE-LCY | CHARGE/FEE-FCY |
|---|---|---|
| (a) Purchase/sale of TCs transaction over the counter | NA | NA |
| (b) Purchase of foreign cheque | NA | NA |
| (c) Sale/purchase of cash passport | NA | NA |
| (d) Telegraphic transfer | | |
| -Inward Telegraphic Transfers [FTIN] | US$ 30 | US$ 30 |
| -Outward International TT / Electronic [ROCT] | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 | 0.25% of transfer, Min US$ 60.00 and Max US $ 500.00 |
| (e) Telex/SWIFT | NA | NA |
| (f) Transfer from foreign currency denominated account to local current | NA | NA |

**5.0 Personal Loans**

| | | |
|---|---|---|
| (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | |
| (i) Personal loans | NA | NA |
| (ii) Overdrafts | NA | NA |
| (iii) Mortgage finance | NA | NA |
| (iv) Asset finance | NA | NA |
| (b) Unpaid loan instalment | NA | NA |
| (c) Early repayment | NA | NA |
| (d) Valuation fees | NA | NA |
| (e) Other | NA | NA |

**Additional Disclossures**

1

| Deposit Rates | LCY | FCY |
|---|---|---|
| -Current Account Deposits | 0%-2.5% | 0%-0% |
| -Time Deposits | | |
| (a) 1 - Months | 2.1% -2.3% | 1.51%-1.67% |
| (b) 3 - Months | 2.47% -2.77% | 1.88%-2.09% |
| (c) 6 - Months | 2.26% -2.56% | 2.32%-2.58% |
| (d) 9 - Months | 3.33% -3.63% | 2.52%-2.79% |
| (e) 12 - Months | 4.40% -4.70% | 2.71%-3.01% |

2

| Lending Rate | LCY | FCY |
|---|---|---|
| Base lending rate | 8.06%-9.06% | 4.8%-5.8% |
| Short term ( up to one year ) | 8.06%-9.06% | 4.8%-5.8% |
| Medium term ( 2 to 3 years ) | 8.56%-9.56% | 5.30%-6.30% |
| Long term ( 3 - 5 years ) | 9.06%-10.06% | 5.8%-6.8% |
| Term loans ( over 5 years ) | 10.06%-11.06% | 6.3%-7.3% |

**6.0**

| Trade Finance Transactions | CHARGE/FEE |
|---|---|
| **Documentary Collections** | |
| Imports | Handling: $130, Acceptance $65, Telex: 0.325% minimum $98 and maximum $650 |
| Exports | All in fee: $100 ($50 courier and $50 handling) per set of documents |
| **Imports Letters of Credits** | |
| Opening fees | LC issuance - 0.5% per quarter Min. $325 |
| Handling fees | Handling: $130 |
| Amendment Fees | Simple amendment $100, extension 0.5% per quarter if it extends to other quarter (s) |
| Confirmation fees | Confirmation 0.39% per quarter Min. EUR 390 per quarter |
| Risk margin on Acceptance | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Other Bank LC re-issuance | 0.1% per Quarter, min. $200 |
| Bills Availization (Pour Aval) | 0.5% per Quarter or part thereof |
| **Exports Letters of Credits** | |
| Handling fees | $500 |
| Courier | $100 |
| Confirmation fees | 0.25% per Quarter or part thereof |
| Negotiation fees | 0.1% Min. $1000 |
| **Liquidity financing** | |
| Suppliers finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| Accounts Receivable Finance | Prevailing market rates and negotiable based on riskness of the transaction |
| **Guarantees and Standby Letters of Credits** | |
| SBLC | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Bid Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Performance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Maintanance Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Advance Payment Guarantee | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Amendments fees on Guarantees | Simple amendments $100 and 0.5% per Quarter or part thereof, if it extends into next quarter(s) |
| Custom Bonds | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Warehouse Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Transit Bond | 0.5% per Quarter or part thereof |
| Facility fees | 1.5% per annum |

We the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information

| | Name | Designation | | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Iddi Msonga | CFO | ........................................................ | Date : 28th July 2022 |
| 2 | Michael Mungure | TTS Head | ........................................................ | Date : 28th July 2022 |
| 3 | Magdalena Martin | Act. Head of Treasury | ........................................................ | Date : 28th July 2022 |

216967401

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mjadala wa mishahara ufike mwisho sasa

**SUALA** la nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma bado limebaki kuwa mjadala, huku pande zote zikieleza namna zinavyolifanyia kazi suala hilo.

Mjadala uliibuka mwanzoni mwa wiki hii kwenye mitandao ya kijamii baada ya kuonekana kile kinachoelezwa ni kiwango cha nyongeza kwa watumishi hao.

Kwa mujibu wa nyaraka hiyo ambayo baadaye serikali ilifafanua kuhusu kiwango cha nyongeza pekee, ilionekana mfanyakazi wa kima cha chini aliongezewa Sh.70,000 na wale wa juu waliongezewa Sh. 20,000.

Msemaji wa Serikali na Mkurugenzi wa Habari Maelezo, Gerson Msigwa, hata hivyo, aliwataka watumishi kuwa watulivu kwa kuwa serikali itafafanua juu ya suala hilo.

Alipozungumza na waandishi wa habari alisema serikali imepokea ombi la Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA), kukutana kabla ya kufanya kikao na upande wa serikali.

Kwa upande wao TUCTA walisema wamewasilisha hoja zao serikalini hususan za nyongeza ya mishahara huku likipendekeza kiwango cha kima cha juu mshahara kisipungue.

Walisema waliona kiwango cha chini ni asilimia 23.3 lakini wa kima cha juu ama asilimia 0.6, huku wakisema ni tofauti kubwa ambayo haijawahi kutokea. Aidha, walisema kuna wengine wenye mishahara binafsi, taasisi na mamlaka za serikali hawakuguswa na ongezeko hilo, jambo ambalo siyo sawa na kuiomba serikali kuliangalia kwa namna ya pekee.

Pia alisema watumishi wa idara za afya, watendaji wa kata na mitaa hawajaguswa na nyongeza hiyo na kwamba kwa kuwa na matabaka kutasababisha mgawanyiko na kushusha morali ya kazi kwa watumishi.

TUCTA ilipendekeza mishahara kuongezwa kama ilivyokuwa inafanyika miaka ya nyuma kwa kutazama asilimia kuliko kiwango cha mshahara wa mhusika, huku wakipendekeza kima cha juu kuongezewa asilimia 15.

Kwanza tunaipongeza serikali kwa kutimiza ahadi yake ya kuongeza mshahara kwa watumishi wa umma, ambao wamekaa zaidi ya miaka mitano bila nyongeza. Pili, utayari wa serikali kukutana na TUCTA hasa baada ya nyongeza hiyo kutokana na upande huo kuonyesha mambo ambayo wanaona hayako sawa wakitaka hatua zichukuliwe kuboresha.

Tunaamini pande zote zitakutana na kujadili kwa kina suala hilo ili lisiwe mjadala bali liingie kwenye utekelezaji na watumishi wawekeze nguvu kwenye kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Ni muhimu sana mchakato wa kuongeza mshahara ukawa shirikishi kwa vyama vya wafanyakazi ili kuepusha malalamiko baada ya kiwango kuwekwa hadharani au kuvuja mtandaoni kama ilivyotokea hivi sasa.

Kunapokuwa na nyongeza ya mshahara inaongeza morali ya kufanyakazi hasa kwa ambaye amekaa muda mrefu bila kuongezewa fedha yoyote kwa wakati ambao nchi ilisema imeelekeza nguvu kwenye ujenzi wenye manufaa kwa watu wengi.

Wapo watumishi wa sekta binafsi wana malalamiko ya kutolipwa, kutokuwa na mikataba wala matibabu ilhali nao ni Watanzania ambao wanalipa kodi kupitia bidhaa na huduma mbalimbali ambayo hutumiwa kulipa na kuendesha serikali.

Mabadaliko ya kutaka kuona watumishi wa umma wanakuwa na maslahi bora yaende hadi sekta binafsi kwa kupitia mikataba ya ajira, matibabu na stahiki nyingine ambazo zipo kisheria, ili kuepusha kuwa na watu wanaoumia lakini wanakosa wa kuwatetea.

Tunatambua watumishi wa umma ndiyo wanachama wa vyama vya wafanyakazi wengi wa sekta binafsi sio wanachama, hivyo wakati mwingine haki zao zinaminywa kwasababu ya kukosa mtetezi, ni muhimu serikali ikaangalia waajiriwa wote ili kuwa na maana halisi ya siku ya wafanyakazi nchini, ikiwezekana isiwe hiari kwa waajiri bali lazima kushiriki.

Bila ukaguzi wa mara kwa mara kwenye sekta binafsi kutatoa picha kuwa wako kwa ajili ya wafanyakazi wa serikali pekee licha ya sheria kuwapo, huku nao wakilipa kodi mbalimbali ambazo zinasaidia kuendesha nchi.

Majadiliano yanayohusu wafanyakazi yasitazame sekta ya umma pekee, bali binafsi ambayo ndiyo imeajiri Watanzania wengi ambao wanalipa kodi na wana mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunakuomba Waziri Aweso, hili la shida ya maji Mwanza limetuelemea



Na Anthony Gervas, Mwanza

**KAULIMBIU** ya 'Maji ni Uhai' bado inakabiliwa na changamoto lukuki kufikia malengo ya kuondoa tatizo la maji katika Jiji la Mwanza na wilaya zake.

Hakuna mtu asiyefahamu kaulimbiu hiyo, lakini kuna shida mahali katika kuhakikisha tatizo hilo ama linaondoka au kupungua na wananchi wanapata maji ya kutosha, badala ya kuendelea kuwapo kilio kile kile kila kukicha katika maeneo mbalimbali ya wakazi wa jiji hilo.

Pamoja na kuwapo Ziwa Victoria ndani ya maisha yetu, sehemu kubwa limezunguka Mkoa wa Mwanza kwenye miji na wilaya ziliko, bado tunakabiliwa na changamoto kubwa ya maji.

Mbali na hapa, ziwa hilo ni chanzo kikuu cha maji katika mikoa jirani hata pakabatizwa jina la Kanda ya Ziwa. Ni mahali Ziwa Victoria lina uwezo wa kuhudumia sehemu kubwa ya nchi, lakini maajabu ya watendaji wetu shida hiyo haiishi kila mwaka, kiangazi kikiwadia vilio vikubwa vya wananchi ni maji.

Maeneo mengi maji huwa hayatoki katika mabomba yao na wengine kulazimika kutumia ya visima virefu na vifupi wakipanga foleni za ndoo. Inakuwa jambo la kustaajabisha sana kuambiwa hadithi za uhaba wa huduma hiyo. Sababu ni nyingi tunapewa, kila siku mpya.

Je, kusingekuwapo chanzo hicho cha maji ingekuwaje sasa? Kwa maana ile Mwanza haipishani na mikoa mingine ambayo haina ziwa kama hili. Mikoa mingine inatumia maji kutoka vyanzo vya visima virefu, vifupi, mito na mabwawa. Kimsingi, ukijiuliza hatupishani nao katika shida hiyo, jambo ambalo haliingii akilini kwa mwananchi wa kawaida.

Hivi, kwanini baadhi ya watendaji mmekuwa mkiingiza siasa kwenye suala nyeti kama hili? Tunapata mtihani hata kutamka 'Maji ni uhai.'

Mfano mdogo Wilaya ya Magu ziwa liko karibu, lakini wananchi kila leo wanalalamikia uhaba wa maji, tatizo hilo limekuwa la kihistoria, ukiwamo mji mdogo wa Kisesa, ambao unahudumiwa na wasimamizi wa maji Mwauwasa kutoka jijini hapa.

> **Mfano mdogo Wilaya ya Magu ziwa liko karibu, lakini wananchi kila leo wanalalamikia uhaba wa maji, tatizo hilo limekuwa la kihistoria, ukiwamo mji mdogo wa Kisesa, ambao unahudumiwa na wasimamizi wa maji Mwauwasa kutoka jijini hapa.**

Bado wako kwenye enzi za zamani za kupanga ndoo foleni visimani na ndoo, baadhi yao maji hayatoki kwenye mabomba yao. Ni hali inayozua malalamiko mengi kwa wananchi wa mji huo wakiitupia lawama mamlaka husika.

Siwabezi ndugu zangu, Wizara ya Maji, lakini naamini mko mashahidi mnalijua hilo. Wananchi inafikia hatua wanaona hakuna maana ya kuwapo chanzo kama Ziwa Victoria, halafu huduma katika maeneo mengi inasuasua, kwanza ni aibu kuwaeleza watu, eti maji ni shida jijini hapa.

Ukweli katika Jiji la Mwanza siku zote, huwa hakuna maji ya uhakika ya bomba, hata kwenye nyumba za kulala wageni zilizo nyingi, maji wanayotumia wateja yanakuwa yamechotwa na kutunzwa kwenye ndoo ya kuogea au jaba. Sababu kuu hakuna uhakika wa kuwapo maji bombani.

Nayasema haya hadharani, kwa sababu nayafahamu na mamlaka wizarani mkitaka kuyashuhudia, mje kimya kimya mshuhudie wananchi wanaumia kubaki na msamiati wa mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.

Hivi karibuni Waziri wa Maji, Juma Aweso, ulizuru jijini Mwanza kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji Wilaya ya Nyamagana na maeneo mengine ya Jiji hilo. Sijua kama ulitazama kwenye wilaya zetu kushuhudia matatizo yanayosibu mitaani kwetu, kwenye wilaya za mkoa huo. Pamoja na wizara yenu kusema inaupiga mwingi katika miradi ya maji, binafsi nasema Mwanza hamuitendei haki. Acheni kusikiliza sifa za wapambe mitandaoni wakati wapo wananchi wengi huku wakiumia na maisha yao.

Tunakuomba Waziri Aweso, ondoa aibu za kukosa maji kutoka bombani, licha ya kuwapo na matatizo mengine ya kitaalamu, pampu za maji, watendaji wako wa chini wasikufiche, wakueleze ukweli wa hali halisi, kazi ya maboresho ifanyike.

TANGAZO

# MUCOBA BANK PLC

P. O. Box 147, Tel. 026-2772165, Fax 026-2772075
Mafinga, Tanzania.

"Kwa Maendeleo Yako"

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30-06-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya/Mwaka wa sasa 30/06/2022 | Robo Mwaka/Mwaka iliopita 31/03/2022 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslim | 462 | 365 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu Ya Tanzania | 181 | 1 |
| 3 | Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio katika Benki Nyingine na Taasisis za Fedha | 2,534 | 2,003 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizo afikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizo kubalika | - | - |
| 9 | Mikopo iliyotolewa kwa Benki nyingine | - | - |
| 10 | uwekezaji katika Amana nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 15,726 | 14,693 |
| 12 | Mali nyingine | 4,401 | 4,090 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa. | 532 | 528 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **23,837** | **21,681** |
| | | | |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisis za Fedha | 3 | 303 |
| 18 | Amana za Wateja | 14,940 | 13,553 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 117 | 117 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Benki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 124 | 272 |
| 24 | Dhima la Tozo KWA Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi. | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 680 | 847 |
| 28 | Madeni | 3,426 | 2,427 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **19,290** | **17,519** |
| **30** | **MALI(DHIMA) HALISI (16 Kutoa 29)** | **4,547** | **4,162** |
| | | | |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | 8,789 | 8,789 |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | - | - |
| 32 | Akiba ya Mtaji | | |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (4,558) | (4,558) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 203 | (183) |
| 35 | Akaunti nyingine za Mtaji | 113 | 113 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | | |
| 37 | **JUMLA YA FEHDA ZA WANAHISA** | **4,547** | **4,162** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | | |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,451 | 1,513 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 160 | 727 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | | |
| | | | |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Amana | 19.08% | 19.19% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo ghafi | 9.90% | 10.30% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 109.25% | 110.36% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 65.97% | 67.77% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zilizozalisha na Jumla ya Mali | 87.69% | 92.45% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 7.78% | -14.85% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 9.95% | -10.74% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/06/2022 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/06/2021 | Limbikizo lamwaka sasa 30/06/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (mwaka uliopita) 30/06/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 943 | 970 | 1,529 | 2,046 |
| 2 | Gharama za Riba | (176) | (230) | (323) | (460) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | 768 | **740** | 1,206 | 1,585 |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | | | | |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 9 | (17) | (213) | (182) |
| | | - | - | - | - |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | 234 | 200 | 457 | 315 |
| | 6.1 Faida/ (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 217 | **194** | 439 | 303 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 18 | 6 | 12 | 12 |
| **7** | **Gharma Zisizo za Riba:** | (625) | **762** | **(1,247)** | (1,354) |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (361) | (379) | (712) | (674) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (24) | (45) | (47) | (78) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (240) | (338) | (488) | (601) |
| 8 | **Faida/ (Hasara) ya Uendeshaji** | 386 | 161 | 203 | 365 |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (30) | (30) | (60) | (60) |
| 10 | **Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | 356 | 131 | 143 | 305 |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | 356 | **131** | **143** | **305** |
| 13 | Idadi ya waajiriwa | 49 | 60 | 49 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 10.88 | 4.93 | 4.38 | 11.17 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na wastani wa mali | 1.69% | 0.73% | 0.89% | 1.65% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya kodi na wastani wafedha za wanahisa | 8.85% | 4.05% | 4.66% | 9.17% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya riba na mapato ghafi | 53.11% | 65.12% | 62.80% | 57.32% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya riba na wastani wa mali zinazozalisha | 4.27% | 6.61% | 1.13% | 8.93% |

Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho
kwa mwezi inayohusika katika kipindi na kugawanywa kwa idadi ya mwezi katika kipindi hicho

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31-03-2022
(Kiasi cha shilingi milioni)

| | Mtaji wa hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2022** | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,344** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 203 | - | **203** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na Wanahisa | - | - | - | **-** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,795** | **(4,355)** | **107** | **4,547** |
| | | | | |
| **Mwaka Uliopita 2021** | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 8,886 | (5,280) | 87 | **3,693** |
| Faida/ (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | 743 | - | **743** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | (91) | - | - | **(91)** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | (20) | 20 | **-** |
| Tengo la ziada ya Jumla | - | - | - | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,795** | **(4,558)** | **107** | **4,345** |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30-06-2022
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya mwaka sasa 30/06/2022 | Robo ya Mwaka iliyopita 31/03/2022 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30/06/2022 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka uliopita) 30/06/2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za uendeshaji** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 356 | (183) | 173 | 305 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | | |
| | Hasara Katika Mali | 39 | 265 | 304 | 534 |
| | Badiliko Halisi Katika Mikopo | (1,042) | 135 | (907) | (1,722) |
| | Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana | 1,087 | (2,437) | (1,350) | (605) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | Mabadiliko halisi Katika Dhima Nyingine | (286) | 111 | (173) | (237) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (312) | 450 | 138 | (288) |
| | Kodi Iliyolipwa | (30) | (30) | (60) | (60) |
| | Mengineyo (Bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli Zauendeshaji** | **(188)** | **(1,688)** | **(1,875)** | **(2,073)** |
| | | | | | |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio lililopokewa | - | - | | |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (4) | (4) | (9) | (35) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya mali zakudumu | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Amana zisizoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya amana Zisisoshughulikiwa na mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(4)** | **(4)** | **(9)** | **(35)** |
| | | | | | |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na shughuli za kifedha** | - | - | (100) | (100) |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | (100) | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutoka na Utoaji wa mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | 1,000 | 20 | 1,020 | |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) Kwa shughuli zakifedha Kifedha** | **1,000** | **(80)** | **920** | **(100)** |
| | | | | | |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu.** | | | | |
| | Ongezeko /Punguzo Halisi Katika | | | | |
| | Fedha taslimu na mali zinazofanana na fedha taslimu | 807 | (1,773) | (964) | (2,208) |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,369 | 4,142 | 4,142 | 4,714 |
| | Fedha na Mali zinazofanana na fedha taslimu mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,177 | **2,369** | **3,177** | **2,506** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA

Katika Kuandaa taarifa hizi za fedha, Sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita ( kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji wa taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina Na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Philip Raymond<br>Meneja Mkuu | (Imesainiwa) | 23/Jul/2022 |
| Kelvin Mushi<br>Meneja wa kitengo cha Fedha and Utawala | (Imesainiwa) | 23/Jul/2022 |
| Saleh S. Abdallah<br>Mkaguzi Mkuu wa Ndani | (Imesainiwa) | 23/Jul/2022 |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunadhibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa za uwasilishaji wa taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya benki na taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonyesha hali halisi

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Arafat A. Haji<br>Mwenyekiti wa bodi ya wakurugenzi | (Imesainiwa) | 23/Jul/2022 |
| 2. Bakar R. Bakar | (Imesainiwa) | 23/Jul/2022 |

### DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2015

### MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| SAVINGS ACCOUNT | CHARGES AND FEES |
|---|---|
| **Individual Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account (GS09)** | |
| Account opening minimum amount | Free |
| Minimum operating balance | Free |
| Minimum Interest Bearing balance | N/A |
| Cash Withdrawal Fee | Refer cash withdrawal fee below |
| Credit Interest Rate | N/A |
| | |
| **Joint Savings Account** | |
| Account opening minimum amount | 20,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Credit Interest Rate | 2% |
| | |
| **Juvenile's/ Minor Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Biashara Savings Account** | |
| Account Opening minimum amount | 65,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 50,000 |
| Monthly Service Fee | 5,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Group Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 10,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee 500 (SMS Alert 1,000) | 1,800 |
| Interest Rate | |
| | |
| **Saccos Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 55,000 |
| Minimum operating balance | 50,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 100,000 |
| Monthly Service Fee | 2,000 |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Elimu Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 10,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 10,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | 2% |
| | |
| **Malengo Savings Account** | |
| Account opening Fee | Free |
| Account Opening minimum amount | 5,000 |
| Minimum operating balance | 5,000 |
| Minimum Interest Bearing balance | 20,000 |
| Monthly Service Fee | Free |
| Interest Rate | See Table below |
| Prematurity withdrawals | 10,000 |

**Malengo account interest rates are as follows:**

| Period | Rate |
|---|---|
| 3 months | 4% |
| 6 months | 5% |
| 12months | 6% |

**FIXED DEPOSIT ACCOUNTS**

| Period | Range | Rate |
|---|---|---|
| 3 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 4.00% |
| 6 months | Up toTzs 9,999,999.00 | 4.50% |
| 9 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 5.00% |
| 12 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 6.00% |
| 24 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 7.00% |
| 36 months | Up to Tzs 9,999,999.00 | 8.00% |

FDR of Tzs**10,000,000** and above is **negotiable** at management discretion.

**GENERAL CHARGES AND FEES**

| GENERAL CHARGES/ FEES | TZS |
|---|---|
| | |
| **Dishonored/Unpaid cheque** | |
| Fund related | NA |
| Technical | NA |
| | |
| **DEPOSIT/WITHDRAWAL TRANSACTIONS** | |
| Cash deposit at branch | Free |
| Cheque clearing (up to Tzs 1,500,000) | 15,000 |
| Cheque clearing (above Tzs 1,500,000) | 1% |
| Cash withdrawal- (less Tzs 5,000,000) | 1,500 |
| Cash withdrawal- from Tzs 5,000,000 and above) | 0.08%, Max Tzs 150,000 |
| Account closure | 10,000 |
| Dormant account reactivation | 5,000 |
| Dormant account monthly Fee | 1,500 |
| Premature/cancelled Fixed Deposit Fee | No interest given |
| Bank Statement Fee /page | 1,200 |
| Audit confirmation Fee | 10,000 |
| Balance certificate Fee | 20,000 |
| Reference Letter | NA |
| TT Outward local-TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| TT Inward local- TISS | NA |
| TT Outward local- EFT | NA |
| Salary Processing (per entry) | 2,500 |
| Bank Guarantees | NA |
| Balance Inquiry | 200 |
| Money Transfer | 15,000 |
| ATM card Cost | 15,000 |
| Searching Fee | 10,000 |
| Coins deposit fee | 10% |
| ATM card replacement | 10,000 |
| ATM w/drawal Fee (on us) | 1,300 |
| To other bank ATMs w/drawal Fee | 1,300 |
| ATM mini statement | |
| Wallet to Bank | 1,000 |
| SMS alart | 500 |
| Bank to Wallet (Below Tzs 100,000) | 1,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 100,000-199,999) | 1,300 |
| Bank to Wallet (Tzs 200,000-299,999) | 1,700 |
| Bank to Wallet (Tzs 300,000-399,999) | 2,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 400,000-499,999) | 2,500 |
| Bank to Wallet (Tzs 500,000-599,999) | 3,000 |
| Bank to Wallet (Tzs 600,000-699,999) | 3,500 |
| Savings account interest rates | 2% |
| ATM Balance Inquiry | 200 |

**LOAN CHARGES AND COMMISION**

| S/NO | CHARGIES |
|---|---|
| 1. | -Loan processing fee 2%<br>-Loan application fee 20,000/= |

216967001

# Mwalimu amuua mkewe kisha kujinyonga

**Na Neema Hussein, KATAVI**

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Tanga, Emmanuel Jerome (32), anadaiwa kumnyonga mke wake katika nyumba ya kulala wageni kisha na yeye kujinyonga kwa kutumia kamba aina ya manila aliyoifunga juu ya mti.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Jerome ni mkazi wa Tanga na chanzo cha tukio hilo ni wivu wa kimapenzi. Makame alisema Jerome alikuwa na mgogoro na mke wake na alikuwa akimtuhumu kuwa na uhusiano wa kimapenzi na wanaume wengine.

Alisema wanandoa hao walipanga safari kwenda mkoani Rukwa ambako ni nyumbani kwa mkewe na walipofika walifikia nyumba ya kulala wageni, ndipo alipochukua uamuzi wa kumnyonga mke wake.

Kamanda Makame alisema Jerome baada ya kumnyonga mkewe, aliacha ujumbe wa maandishi kwa ndugu wa mke wake, ambao ni shemeji zake uliosomeka: "Nisameheni kwa yalitokea".

Alisema Jerome baada ya kufanya tukio hilo mkoani Rukwa, alikimbilia mkoani Katavi na Julai 27, mwaka huu, na kufikia katika mtaa wa Ilembo Manispaa ya Mpanda ambako alichukua uamuzi wa kajinyonga.

Katika hatua nyingine, Jeshi la Polisi linamshikilia Kisabo Ngabezuri (43) kwa madai ya kufanya mauaji ya Nagala Ilasa (45) kwa kumchoma kisu sehemu mbalimbali za mwili wake.

Kamanda Makame alisema Ilasa alifariki dunia Julai 26, mwaka huu, wakati akipatiwa matibabu hospitalini. Tukio hilo linadaiwa kutokea katika Kijiji cha Mapili Wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Alisema Julai 25, majira ya saa 4:00 usiku, ulitokea ugomvi baina ya Ngabezuri na Ilasa wakiwa kilabuni wanakunywa pombe.

Makame alisema wanaendelea kumhoji mtuhumiwa ili kuwapata wengine waliokuwapo katika ugomvi huo kisha kuwafikisha mahakamani.




Meneja wa Biashara ya Kadi wa Benki ya NBC, Esnat Hollela (wa tatu kushoto), akipeana mkono na Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa na Mauzo wa benki hiyo, Abel Kaseko, wakati wa uzinduzi wa huduma ya kadi ya malipo ya Dola inayowezesha malipo mtandaoni bila makato ya ziada, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja wa Bidhaa na Mauzo wa benki hiyo, Dorothea Mabonya na Kaimu Mkuu wa Huduma za Kidigitali Ulrik Peter. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Tanzania yapiga hatua mikopo ya nyumba

**Na Munir Shemweta**

TANZANIA imepiga hatua katika utoaji mikopo ya nyumba huku ikibainika kuwa mikopo 6,182 imetolewa hadi sasa ikilinganishwa na 579 iliyotolewa hadi kufikia mwaka 2009.

Licha ya ongezeko la mikopo hiyo, pia muda wa urejeshaji umeongezeka kutoka miaka 15 hadi 25 sambamba na riba za mkopo kupungua kutoka asilimia 20 hadi 22 mwaka 2009 hadi asilimia 15 hadi 19 zinazotozwa sasa.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula juzi, 2022 katika Mkutano Mkuu wa 41 wa Taasisi ya Shelter Afrique unaoendelea Victoria Falls, Zimbabwe ambapo Tanzania inahudhuria kama mwanachama.

Akichangia mada kuhusu jukumu la Benki Kuu kwenye soko la nyumba katika Bara la Afrika huku akitoa uzoefu wa Taasisi ya Tanzania Mortage Refinance Company' iliyoanzishwa kutokana na utekelezaji wa mradi wa mikopo ya nyumba uliokuwa ukisimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dk. Mabula alisema kumekuwa na mafanikio makubwa toka kuanzishwa taasisi hiyo.

Alisema kwa sasa benki na taasisi za fedha 33 zinatoa mikopo ya nyumba tofauti na ilivyokuwa kabla ya kuanzishwa kwa taasisi hiyo ambapo awali benki tatu tu ndizo zilizokuwa zikitoa mikopo.

Waziri Mabula aliwaeleza washiriki wa mkutano huo umuhimu wa Benki Kuu kusimamia ipasavyo benki na taasisi zinazotoa mikopo hiyo ili kuhakikisha zinatoa riba ambazo wananchi wanaweza kumudu kwa kuwa nazo zinawezeshwa kupata mitaji nafuu.

Kuhusu upungufu wa nyumba 3,000,000 na mahitaji ya nyumba 200,000 kwa kila mwaka nchini Tanzania, Dk. Mabula alisema endapo benki na taasisi za fedha zitaendelea kuachiwa kutoza riba kubwa bila usimamizi, haitafanikiwa kuwezesha wananchi hususan wa kipato cha chini kumudu gharama za nyumba bora.

"Endapo benki na taasisi za fedha zitaendelea kuachiwa kutoza riba kubwa bila usimamizi, itakuwa vigumu kuwezesha wananchi hususan wa kipato cha chini kumudu gharama za nyumba," alisema.

Mkutano Mkuu wa 41 wa Shelter Afrique ulioanza Julai 25, unatarajiwa kumalizika leo na unahudhuriwa na nchi wanachama wa bara la Afrika ikiwamo Tanzania na umebeba kaulimbiu ya 'Climate Change and the Built Environment'.


**CRAIG DORIA SAFARIS LIMITED (VOLUNTARY LIQUIDATION) COMPANY NO 52157**

**NOTICE OF FINAL MEETING**

**IT IS HEREBY NOTIFIED THAT** pursuant to section 345 of the Companies Act 2002 the meeting of the members for the purpose of lying down the accounts and giving any explanations thereof with respect to the voluntary winding up of Craig Doria Safaris Limited (the Company) will be held on 11th day of January, 2022. The meeting will be held at the registered office of the Company at **PLOT NO FARM NO 17, STREET NGOROBOB HILL, WARD MATEVES, ROAD A TO Z, DISTRICT ARUSHA, REGION ARUSHA.** The agenda of the meeting will be laying of the account of winding up of the company and giving any explanation thereof on closure of the Company. If any person has any interest, they are advised to contact the liquidator at the address below within thirty (30) days of this notice.

LIQUIDATOR
WILFRED SAWAYA MAWALLA

**KUPOTEA KWA VYETI**



**JOSEPH ELIAS MBOWE** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **BACHELOR OF SCIENCE WITH COMPUTER SCIENCE** chenye usajili namba **23652/T.98** chenye namba **BSCWCOM 000008** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM mwaka 2001** na cheti cha chuo cha **MASTERS IN COMPUTER SCIENCE** chenye usajili namba **P 065/T.12** kilichotolewa na **UNIVERSITY OF DAR ES SALAAM** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kwenye kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: UD/RB/3726/2016**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu **VITALISI LUCAS YELINDE** anatangaza kupoteza kadi ya gari namba **T149DVQ** aina ya Toyota Probox.Taarifa imetolewa kituo cha Polisi Bukoba kwa **RB** namba **KAG/BUK/RB/298592/2022.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**RODGER FARREN RODGER** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA LAND CRUISER PICK UP YENYE NAMBA ZA USAJILI T376 AED KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
**TAARIFA:-**
**ARU/ARU/RB/289180/2022**

**KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

**FARAJA JOHN MTEGA** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya pikipiki aina ya Sinoray yenye namba za usajili **MC316 CTS,** Chasis namba **LD3PCK6J9L2014209** na Engine namba **SR162FMJ20094086** Kwa yeyote atakayeiona au kuiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
**Taarifa ya polisi: MAN/BAB/RB/296911/2022**

**KUPOTEA KWA VYETI**



**YUSUPH KISEO NZOWA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **CS16000217537** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya **EAGLE SECONDARY** mwaka **2015**,na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **ACS19080193** kilichotolewa kupitia shule ya **ALPHA SECONDARY** mwaka **2019**, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/298218/2022**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

1: Shauri la Talaka Na.26/2016
**Mdai:** Grace Abraham Mwakibete
**Mdaiwa:** Clement Philipo Fungo
2.Misc.APPL. Na.37/2020
**Mdai:** The Registered Trustees of Pentecostal Minission(PHM)
**Mdaiwa:** Pastor Ezekiel Kalinga
Kwa mamlaka tuliyopewa na Mahakama ya Mwanzo(W) Bomani/Iringa na Baraza la Ardhi na Nyumba(W) Iringa, tutauza kwa Mnada wa hadhara nyumba mbili(2) za makazi tarehe 02/08/2022, saa tano(5:00) asubuhi kama ifuatavyo:

1. Nyumba na viwanja viwili(2) vya wanandoa: Grace Abraham Mwakitebe na Clement Philipo Fungo mali zote zipo Ngelewala /Mwangata/Iringa nyumba Na. IMC/A.10/43/141 squatter area.
2. Nyumba ya mdaiwa Pastor Ezekiel Kalinga iliyopo Kivukoni/Mtua/Ilula//Kilolo katika eneo lisilo pimwa(squatter area).

**Masharti:** Mnunuzi anatakiwa kulipa 25% papo hapo na salio alipe ndani ya siku kumi na nne(14) na akishindwa kulipa mali itauzwa tena kwa mnada wa hadhara na malipo ya awali hayatarudishwa.
UTAWALA
**WASILIANA NASI KWA NAMBA: 0755 976 676/0767 969 133.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**
**Shauri la Madai Na. 28/2022**
**Jina la Mdai.................PENDO CHARLES**
**Jina la Mdaiwa..................ELISHA JAPHET**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: ELISHA JAPHET**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake ya TALAKA PAMOJA NA KUACHANA**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 04 Mwezi 08 Mwaka 2022 saa 2:00 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 25 Mwezi 07 Mwaka 2022.

HABARI KITAIFA

# Serikali yaahidi kulinda mazingira ya bahari kwa rasilimali endelevu

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeahidi kuendeleza jitihada za kulinda mazingira ya bahari ili rasilimali zinazopatikana humo ziwe endelevu.

Ahadi hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula.

Aliyasema hayo wakati akifunga kongamano la siku tisa la wataalamu kutoka mataifa 21 kuhusu mikakati ya kuhakikisha mazingira ya bahari yanaendelea kuwa safi, lililoandaliwa na Umoja wa Mataifa.

"Tumefarijika sana Umoja wa Mataifa wameona umuhimu wa kufanya kongamano kama hili la kuangalia namna ya kuzingatia mazingira ya baharini hapa Tanzania, tunaahidi kuendelea kutunza mazingira ya bahari kwa manufaa yetu," alisema Mulamula.

Alimpongeza Balozi wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa, Gaston Kenendy kwa kushawishi mkutano huo muhimu kufanyika Tanzania.

Aidha, Balozi Mulamula alisema mkutano huo umekuja wakati mwafaka ambapo Tanzania itashirikiana na Umoja wa Mataifa kulinda mazingira ya bahari ili kuwa na rasilimali endelevu kwa maslahi ya vizazi vijavyo.

Alisema kwenye mkutano huo wataalamu hao walizungumza namna mataifa yanavyoweza kutumia rasilimali zinazopatikana baharini kuleta maendeleo endelevu bila kuathiri mazingira yake na viumbe vilivyoko baharini.

"Katika siku hizi tisa wataalamu hawa wa mazingira wametembelea pia miradi yetu ya kimkakati kuangalia namna tunavyojipanga kuimarisha miundombinu ya usafiri na pia wameenda Zanzibar wamekutana na Waziri wa Uchumi wa Buluu," alisema Mulamula.

Alisema Tanzania inashiriki kwenye mazungumzo na Umoja wa Mataifa kuhakikisha inapata mkataba ukataoziwezesha nchi zote wanachama wa umoja huo kuweka kipaumbele suala la kulinda mazingira ya bahari.

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka, alisema mkutano huo kufanyika hapa nchini ni miongoni mwa fursa chache sana kupatikana.

Alisema muda mwingi NEMC imekuwa ikihangaikia usimamizi wa mazingira kwenye nchi kavu na maziwa lakini kwenye bahari bado walikuwa hawana uelewa wa kutosha hivyo kongamano hilo imekuwa fursa kwao.

"Hili kongamano limetufumbua macho zaidi kujua ni kwa kiwango gani tunapaswa kufaidika na uchumi wa bahari kwasababu tuna rasilimali nyingi za bahari lakini tunanufaika kidogo sasa baada ya hili kongamano tumejua mambo mengi ya kufanya tunufaike na wakati huo huo tulinde mazingira ya bahari," alisema Dk. Gwamaka.



Mbunge wa Bagamoyo mkoani Pwani, Muharami Mkenge, akihutubia mkutano wa hadhara katika Kata ya Mapinga alipokuwa kwenye ziara ya kukagua shughuli za maendeleo juzi. Kulia ni Mwenyekiti wa CCM wa kata hiyo, Hassan Omary na Diwani wa kata hiyo, Dismass Chandika. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanachama wa CCM waonywa kusigana

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Pwani, kimewaonya wanachama wanaojitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kuacha kusigana katika kipindi hiki cha uchaguzi wa ndani wa chama.

Akizungumzia hali ya uchaguzi unaoendelea, Kaimu Katibu wa CCM Mkoa wa Pwani, ambaye ni katibu wa Jumuiya ya Wazazi mkoani hapa, Elisante Msuya, alisema juzi kuwa kuna baadhi ya wagombea ambao wameanza kusigana jambo ambalo ni kinyume cha kanuni.

Kutokana na hali hiyo, Msuya alisema uchaguzi uko katika mfumo, ratiba na taratibu, hivyo wanatakiwa kuzifuata bila kukiuka ili wamalize vizuri.

Alisema zaidi ya wanachama 50,000 wamejitokeza kugombea nafasi za jumuiya na chama katika mkoa wa Pwani.

"Haijapata kutokea wingi huu kuanzia ngazi ya tawi hadi sasa tunapoelekea mkoa wanachama kujitokeza katika nafasi moja watu 20 kitu ambacho hakijawahi kutokea. Tunapata wakati mgumu katika mchujo kwani tunatakiwa kupata watu makini," alisema Msuya.

Kadhalika, Msuya alisema wameshamaliza uchaguzi ngazi ya matawi na sasa wanafanya uchaguzi wa jumuiya hadi juzi walikuwa wamefikia asilimia 95 katika kata 133. Kata sita kati ya hizo zitabaki kutokana na maelekezo waliyopewa kurudia uchaguzi.

Katika hatua nyingine, Msuya alikana kupokea taarifa za viongozi wa chama kuhusishwa kwenye uuzaji wa eneo la ranchi ya Razaba linalomilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

# DC aikaba koo RUWASA alipo mkandarasi wa mradi wa maji

**Na Steven William, IRINGA**

MKUU wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, ametoa saa 48 kwa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) kumlipa mkandarasi wa mradi unaopeleka maji Neghabihi na Ikengeza unaotekelezwa kwa fedha za UVIKO - 19 wenye gharama ya Sh. 643,792,097.

Akiwa katika ziara ya ukaguzi wa miradi ya maji Wilaya ya Iringa juzi, Moyo alisema kazi iliyofanywa na mkandarasi GNMS Contractors kwa kiasi kikubwa imekamilika na kilichobakia ni kulipwa fedha zake.

Moyo alisema haiwezekani mkandarasi amemaliza kazi lakini mhasibu anachelewesha malipo, hivyo akamwagiza Meneja wa RUWASA Wilaya ya Iringa kumlipa fedha mkandarasi huyo.

"Meneja mwambie mhasibu amlipe mkandarasi ndani ya saa 48 kinyume cha hapo atamchukulia hatua za kisheria kwa kuwa kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya ya Iringa imeridhishwa na kazi iliyofanywa na mkandarasi," alisema Moyo.

Alisema mradi umefika asilimia 73 na hakuna malipo yoyote yaliyofanyika, hivyo RUWASA inapaswa kulipa haraka malipo ambayo mkandarasi anadai ili kumalizia kazi iliyobaki hatimaye kuwatua ndoo wanawake.

Meneja wa RUWASA Wilaya ya Iringa, Mhandisi Masoud Samila, alisema mradi huo ni wa teknolojia ya msukumo kwa kutumia pampu ya umeme na chanzo cha maji ni visima virefu kwa maeneo yote mawili ya Neghabihi na Ikengeza.

Samila alisema lengo ni kuwapatia wananchi wa eneo husika majisafi na salama katika umbali usiozidi mita 400 pamoja kupungunza milipuko wa magonjwa mbalimbali yanayoweza kujitokeza kutokana na ukosefu wa huduma ya majisafi na salama.

Alisema mradi huo unatarajiwa kuwanufaisha wananchi 4,920 ambao walikuwa wanakosa majisafi na salama karibu, hivyo kukamilika kwake kutachochea kuongezeka shughuli za kiuchumi kwa wananchi walioko maeneo ya mradi.

# Waziri ataka miradi barabara ilingane na thamani ya fedha

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amewaagiza mameneja wa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara (TANROAD) kuhakikisha miradi yote ya ujenzi wa barabara inayotekelezwa nchini ilingane na thamani ya fedha zinazotolewa na serikali.

Dk. Mwigulu ambaye ni Mbunge wa Iramba Magharibi alisema hayo juzi kwenye kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Singida.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi hii ili kumuheshimisha nawaombeni miradi hiyo mnayoisimamia kuijenga ilingane na thamani ya fedha zinazotolewa na serikali," alisema.

Naye aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, ambaye alikuwa mwenyekiti wa kikao hicho, alisema wataalamu wahakikishe fedha zilizotengwa na serikali kwa ajili ya mkoa huu zinatumika kuleta mabadiliko makubwa kwenye miundombinu ya barabara.

Alisema serikali imetenga fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo na ufunguzi wa barabara mpya ili ziweze kusaidia kuleta maendeleo ya wananchi.

"TARURA na TANROAD mhakikishe fedha zinatumika vizuri kukarabati na kuanzisha barabara mpya katika maeneo yenye changamoto za upitaji ili kukamilisha kauli ya 'Tunawafikisha Pasipo Fikika' inatimia," alisema.

Dk. Mahenge alisema bado kuna maeneo mengi katika mkoa huu ambayo yana changamoto kubwa ya miundombinu ya barabara hivyo ajenda hiyo ni muhimu kujadiliwa kwa kina kwa kuwa ni chombo cha kuleta maendeleo ya wananchi.

Aliagiza TANROADS na TARURA kutenga maeneo katika barabara kwa ajili ya kupitisha mifugo ili kuzitunza na akasisitiza elimu itolewe kwa wananchi ya utunzaji wa barabara hizo.

Mbunge wa Singida Mashariki, Jumanne Mtaturu, alisema pamoja na jitihada za kutengeneza na kufungua barabara mpya lakini kasi ya uharibifu wa barabara hizo imekuwa ikiongezeka sana.

Awali akitoa taarifa, Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Tembo David, alisema mkoa una mtandao wa barabara zenye urefu wa kilometa 5,666.412 kati ya hizo barabara zenye urefu wa kilimeta 1360.6 sawa na asilimia 24 zina hali nzuri na zinapitika majira yote ya mwaka wakati kilomita 1700.8 sawa na asilimia 30 zina hali ya wastani na kilomita 2607.9 sawa na asilimia 46 zina hali mbaya.

Meneja wa TANROADS, Mhandisi Msama Kosani Msama, alisema katika mpango wa bajeti wa mwaka 2022/23 Mkoa wa Singida wamewekа mpango wa kuweka taa za barabarani katika maeneo mbalimbali.

Alitaja baadhi ya maeneo hayo kuwa ni katika barabara inayoanzia ofisi za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) hadi Mwenge katika barabara ya Singida - Gehandu na kuanzia Skyway hadi Kona ya Mohamedi, Njuki hadi Mizani katika barabara ya Dodoma - Singida - Mwanza.

Wakichangia katika kikao hicho baadhi ya wabunge na wenyeviti wa halmashauri za wilaya mkoani hapo waliomba barabara zilizoombwa kujengwa zijengwe kwa wakati.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega ambaye alitaka wilaya hiyo ipewe kipaumbele kwa kuzingatia kuwa haina barabara ya kiwango cha lami inayounganisha wilaya hiyo na makao makuu ya wilaya ukilinganisha na halmashauri zingine.

# Mradi umeme kuleta mageuzi nishati

**Na Mwandishi Wetu**

MRADI wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme ya kV 400 kutoka Iringa hadi Zambia (TAZA) utaanza kutekelezwa Januari, mwakani na kukamilika mwaka 2025.

Mradi huo utawezesha upatikanaji umeme katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Songwe na Rukwa pamoja kuiwezesha Tanzania kufanya biashara ya umeme katika nchi za kusini na mashariki mwa Afrika.

Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema hayo juzi alipofika katika eneo litakalojengwa kituo cha kupoza na kukuza umeme cha Tunduma wilayani Momba, mkoani Songwe. Kituo hicho ni moja kati ya vituo vitano vya kupoza umeme vitakavyojengwa kwenye mradi huo.

Alisema mradi huo una muhimu wa kipekee kwa kuwa unaifanya Tanzania kuwa kiungo cha biashara ya umeme na pia unaipa Tanzania nafasi ya kuendelea kuzalisha umeme zaidi hata utakaozidi mahitaji ya nchi kwa kuwa kuna fursa pia za biashara ya umeme.

"Tuna matumaini mradi utakamilika ndani ya miaka miwili kwani umetengwa katika vipande vinane, hivyo kutakuwa na makandarasi wengi watakaofanya kazi kwa mpigo, hii itawezesha kujengwa kwa vituo vitano vya kupoza umeme pamoja na njia ya kusafirisha umeme kutoka Iringa hadi Rukwa na kipande cha kwenda mpaka wa Zambia," alisema.

Pia katika kutekeleza kipaumbele cha Wizara ya Nishati cha kupeleka umeme kwenye maeneo ya uzalishaji ikiwapo migodi, Waziri Makamba alifika katika Kijiji cha Itumbi, Chunya mkoani Mbeya ili kuzungumza na wachimbaji wadogo na kuwaleeza hatua zilizochukuliwa na serikali za kupeleka umeme kwenye maeneo yao ya uchimbaji, kusikiliza kero zao na kuhamasisha matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia.

Waziri aliwaeleza wachimbaji hao kuwa maeneo 22 ya uchimbaji madini wilayani humo yatapata umeme kupitia mradi wa Gridi Mapato ambao tayari una Sh. bilioni 300 ambazo zitapeleka umeme kwenye maeneo ya uzalishaji ikiwamo migodi na viwanda nchini.

Mratibu wa Mradi wa TAZA, Mhandisi Elias Makunga, alisema mradi huo utatekelezwa kwa gharama ya Sh. trilioni 1.4 ambazo tayari Tanzania inazo na kwamba utakuwa kiunganishi cha kwanza cha umeme wa juu kati ya Nchi Wanachama wa Kusini mwaka Afrika (SAPP) na Nchi Wanachama wa Mashariki mwa Afrika (EAPP).

Alisema kukamilika kwa mradi huo kutachagiza biashara ya umeme kwa kuwa Tanzania itanunua umeme nje ya nchi pale panapokuwa na upungufu na pia itakuwa na uwezo wa kuuza umeme nje ya nchi pale inapokuwa na ziada.

Mhandisi Makunga aliongeza kuwa Sh. bilioni 23.1 zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi 6,198 waliopisha mradi huo na Wizara ya Fedha na Mipango kuanzia Agosti, mwaka huu, itafanya uhakiki ili kila mwananchi apate fidia stahiki kabla ya mradi kuanza.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (katikati), Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Ukanda wa Afrika Mashariki, Nnenna Nwabufo na Ofisa Mtendaji Mkuu wa African Guarantee Fund (AGF), Jules Ngankam, wakionyesha nyaraka za makubaliano baada ya kusaini mikataba miwili yenye thamani ya dola za kimarekani milioni 110, jijini Dar es Salaam juzi, ili kuwezesha mikopo kwa wanawake wajasiriamali wadogo na kwa maendeleo ya wananchi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Ulevi chanzo cha wavuvi kufa maji'

**Na Jenifer Gilla**

ULEVI na ukosefu wa elimu kwa wavuvi vimeelezwa kuwa moja ya vyanzo vya ajali za baharini nchini, hali inayochangia kupoteza nguvu ya taifa.

Hayo yameelezwa juzi na mkufunzi wa mafunzo ya uvuvi wa Wakala wa Elimu ya Mafunzo na Uvuvi Kampasi ya Mbegani, Mwanza wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kuzuia Ajali za Majini yaliyofanyika katika mwalo wa samaki wa Msasani, jijini Dar es Salaam.

Maadhimisho hayo yalifanyika kwa kaulimbiu ya 'Kuzama Kunazuilika Chukua Tahadhari'.

Alisema kuwa utafiti wa mwaka 2017, 2018 na 2019 umeonyesha wavuvi 25 kati ya 40 wametumia pombe na bangi wakiwa baharini kwenye shughuli za uvuvi wakiamini kuwa wanajiepusha na msongo wa mawazo.

"Unajua hizi kazi za bahari ni ngumu, sasa mtu anafikiria kwamba nikienda nimelewa nitakuwa nimepunguza baadhi ya stress (matatizo), kwanza mapato ni kidogo, anaweza akarudi na mzigo wa elfu kumi tu ambayo haigawanyiki hata kwenye familia kwa hiyo wanaona bora walewe," alisema.

Aidha, alisema baada ya kugundua hayo walipata ithibati ya kuzunguka nchi nzima ya kuwafundisha wavuvi madhara ya kiafya na kisheria ya kwenda baharini huku ukiwa umelewa, shughuli wanayoendelea nayo hadi watakapojiridhisha na usalama wa shughuli hiyo.

"Hili tatizo litakwisha kama hawa watu watapata elimu nchi nzima, kwa sababu wavuvi wengi wanaamini kwenda baharini ukiwa umelewa ni kawaida na sehemu ya maisha kama ukiwa nchi kavu. Kumbe baharini ni sehemu hatari sana," alifafanua Nicas.

Kwa mujibu wa mkufunzi huyo, serikali iweke mkakati wa kuwapima wavuvi kabla ya kuingia baharini kubaini kama hawajatumia kilevi kama inavyofanyika kwa madereva.

Ofisa Mwelekezi kutoka Shirika la Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo (EMEDO), Grace Andrew, alisema Watanzania 3,000 kila mwaka wanapoteza maisha nchini kutokana na ajali za kuzama maji.

Alisema wengi hukutwa na mauti wakiwa wanaoga, kukusanya maji kwa matumizi ya nyumbani, kusafiri juu ya maji kwenye boti na uvuvi.

Andrew alisema shirika hilo linaandaa maadhimisho hayo kwa mara ya pili nchini tangu Umoja wa Mataifa (UN), kupitisha Julai 25 kila mwaka kuwa siku maalum ya maadhimisho hayo duniani ili kutoa elimu kwa wadau wa bahari na Watanzania namna ya kujikinga na ajali hizo.

"Aprili 21, mwaka jana, UN ilipitisha siku ya leo kuwa ya maadhimisho ya kuzuia ajali za baharini kwa kuwa iliona kuwa ajali ni nyingi, lakini hazitolewi taarifa na kufanyiwa uhamasishaji. Utafiti uliofanywa na Shirika la Afya Duniani (WHO), unaonyesha watu 3,000 hufa maji kila mwaka hapa Tanzania na 236,000 duniani," alisema.

Naye Katibu wa Kikundi cha Wavuvi Mwalo wa Msasani (KIWAWAM), Ujeje Mamboleo, alisema kila mwezi wavuvi wasiopungua watano wanakufa baharini.

Mmoja wa wavuvi wa mwalo huo, Lucas Gallu alisema: "Mimi ni mhanga wa kuzama dada yangu, miaka ya hivi karibuni nilipata ajali ya kupinduka na boti katikati ya bahari nikiwa na wenzangu wawili, ilituchukua takribani saa 12 kuokolewa na wenzetu. Kwa hiyo maadhimisho haya huwa sikosi ili nijue ni nini hasa serikali imepanga juu yetu."

Akifungua maadhimisho hayo, Katibu Tawala wa Wilaya Kinondoni, Stella Msofe, alisema serikali imepokea malalamiko na mapendekezo kwa ajili ya kuyafanyia kazi.

Ukurasa 13




LATRA mnaupiga wote, lakini pigeni na hapa

BUFE
IJUMAA JULAI 29, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



**TARURA yahesabu orodha ya mafanikio kwa miaka mitano kuanzishwa kwake**

Ukurasa 12

# Tanesco yaanza mpambano na wezi vifaa Shinyanga kupitia Sungusungu

## • Wajibiwa kazi inaanza mara moja

**Na Shaban Njia, KAHAMA**



Ofisa wa Shirika la Tanesco wilayani Kahama, Mhandisi Iddi A. Iddi, akiwaonyesha Sungusungu nyaya aina ya kopa zinazoibiwa zaidi kwenye transfoma. **PICHA: SHABAN NJIA.**

MKOA wa Shinyanga hususani wilaya ya Kahama inatajwa kuwa kinara wa kuharibu miundombinu ya Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hasa wizi wa mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma katika kanda ya Magharibi, ambapo pia kuna mikoa kama vile Tabora, Katavi na Kigoma.

Ni hali ambayo zao lake ni wateja wa Tanesco kuendelea kukosa huduma kwa wakati, viwanda kusimamisha uzalishaji kwa muda usiojulikana, huku shirika hilo nalo mapato yake yakididimia mkoani humo.

Pia, ni wizi unaokwamisha juhudi za shirika kusogeza huduma ya nishati kwa wananchi, hususani kwa wanaoishi pembezoni mwa miji na miradi yao nayo, haikamiliki kwa wakati.

Hapo ndipo Tanesco Kahama, imeamua kushirikisha askari wa jadi, Sungusungu kuchukua jukumu la kulinda miundombinu ya umeme katika maeneo yao, kudhibiti wezi wanaohujumu shirika, wakienda kuuza vitu hivyo kama vyuma chakavu.

Sungusungu hao ni kutoka kata 58 za Halmashauri za Msalala, Ushetu, na Manispaa ya Kahama, pale wanapomuona mtu au fundi anapanda kwenye nguzo za umeme, wahakikishe wanamhoji kujua uhalali wake, pia penye shaka watoe taarifa katika ofisi za Tanesco kujiridhisha.

**OFISA KANDA YA MAGHARIBI**

Ofisa Usalama Kanda ya Magharibi Tanesco, Mhandisi Saidi Songwe, wilaya ya Kahama imekuwa kinara wa kuhujumu miundombinu za umeme, wakiiba mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma, hata kulifikisha shirika hilo kupata hasara ya Sh. milioni 400 hadi sasa.

Anasema hata wateja wao, nao wanaendelea kukosa huduma kwa matumzi ya kawaida na uzalishaji, huku Tanesco inakosa kwa kiasi kikubwa, kutokana na kuhujumiwa vifaa ambavyo ndivyo ulinzi mkubwa wa tansfoma.

Mhandisi Songwe anafafanua, yanapotolewa mafuta na anachokiita 'nyaya za kopa' kwenye transfoma, Tanesco huingia gharama ya Sh.milioni 12 kurekebisha na inapochelewa, hasara ni huwa maradufu, akitoa mfano wa pigo la hasara, Sh.milioni 400 na ndiyo sababu ya kushirikisha Sungusungu kuimarisha ulinzi wa vifaa vyao.

"Serikali inatoa fedha nyingi katika kusogeza huduma ya nishati kwa wananchi, baadhi yao wanaihujumu kwa kuiba nyaya za kopa na mafuta kwenye transfoma ambayo zinasaidia kulinda uhai wa transfoma na kufanya kazi vyema, na wanaenda kuuza kama chuma chakavu," anasema Songwe.

Kwa mujibu wa Songwe, matukio ya wizi wa vyuma katika njia za usafirishaji umeme, yamepungua kwa kiasi kikubwa shida ipo katika wizi wa mafuta na nyaya za kopa kwenye transfoma.

**MENEJA SHINYANGA**

Mhandisi Grace Ntungi, ni Meneja wa Tanesco mkoa wa Shinyanga, anataja wizi wa vifaa hivyo, upo zaidi katika kata za Kagongwa Manispaa ya Kahama, na kata ya Bulyanhulu, katika Halmashauri ya Msalala, hata kuchangia umeme kukatika huko kila mara.

Anasema, mpaka sasa zaidi ya transfoma 40 zimeshaharibiwa kwa kuibwa mafuta na nyaya za kopa zinazolinda uhai wake kufanya kazi. Hapo anaomba msaada mkubwa wa Sungusungu, kudhibiti wizi huo.

Meneja huyo wa Tanesco ana maoni kwamba Sungusungu wahakikishe kuwa mstari wa mbele, kuhakikisha wanatokomeza vitendo hivyo, kwa sababu wahujumu wanaishi yao mtaani, ikiwezekana kukomesha tabia hiyo.

Katika hilo, Festo Kiswaga, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, anawataka sungusungu wote kufanya mikutano katika maeneo yao kuwaleza wananchi haja ya kulinda miundombinu ya umeme.

Hapo inatangazwa, sungusungu atakayemkamata mwizi anayehujumu atapewa zawadi Sh.500, 000 na cheti cha ushujaa, akifafanua lengo kuinufaisha Tanesco, wananchi, pia serikali.

Mkuu wa Wilaya anatoa tahadhari kwamba, itaanza kuwachukulia hatua kwanza makamanda wa Sungusungu. kwani wao ndio wanaishi na wanajamii.

"Mkimkuta mwizi akiwa anahujumu miundombinu ya shirika hakikisheni mnamuwajibisha kisheria na kutoa taarifa kituo cha polisi kwa hatua zaidi za kisheria na mkimkuta amefika kwenye transfoma baada ya kutokea kwa shoti, toeni taarifa Tanesco," anasema Kiswaga.

Anaendelea:"Hawana akili wote wanaohujumu miundombinu, kwa sababubu wanaiba vitu vya gharama kubwa na kwenda kuuza kama chuma chakavu tena kwa fedha kidogo,na kwa mara ya mwisho wezi hao waliiba Transfoma ya Kata ya Kagongwa".

Mwenyekiti wa Sungusungu Wilaya, Muzari Kashindya, anaahidi watahakikisha wanafanya mikutano ya kila mara kukumbushana wajibu wa jeshi lake la jadi, ikiwemo kulinda miundombinu ya Tanesco na anaomba Polisi kuwapa ushirikiano.

Anakiri ni zaidi ya miaka mitatu hawajafanya mikutano ya kukumbushana majukumu yao na wengi walijisahau kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao, hata kuchangia kuibuka wizi wa namna hiyo.

Sungusungu Paul Mabula na Samwel Mpengo, wanaahidi kuingia katika mapambano na watashirikiana na wananchi kuibua wahalifu walioko.

Mpengo anaisihi Tanesco, kuhakikisha wanapopeleka nyaya vijijini kuwafungia huduma wananchi, wawe wanawajulisha zilizosalia ili wao Sungusungu, wahakikishe wanazilinda.

Pia, Mpengo analiomba shirika kuwapatia orodha kamili ya transfoma zilizopo katika Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama, ili waelekeze nguvu za ulinzi huko.

IJUMAA JULAI 29, 2022 BUFE 13

UCHUMI

# TARURA yahesabu orodha ya mafanikio kwa miaka mitano kuanzishwa kwake

## • Yajayo; mradi wa ujenzi bonde Jangwani waja

**Na Mwandishi Wetu**

WAKALA wa Usimamizi wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unaadhimisha miaka mitano tangu uanzishwe, ukiwa na mafanikio lukuki kiasi cha wengine kudhani imekuwepo nchini miaka mingi.

TARURA ilizinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa mnamo Julai 2, ya mwaka 2017, baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali mwezi Mei mwaka huo.

Ni uzinduzi ambao Waziri Mkuu, alitamka katika lugha ya ahadi kwamba, itakabili changamoto ya usafiri nchini, hasa maeneo ya Vijijini yaliyo chini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, ikielekea kumalizika.

"Wakala huu tunaouzindua leo, utakuwa na manufaa makubwa kwa ustawi wa nchi yetu kwa kuongeza chachu ya uzalishaji mali mashambani kutokana na urahisi wa mazao kufika sokoni. Utashusha bei ya vyakula mijini na bidhaa za viwandani Vijijini, kutokana na gharama za usafirishaji mazao kutoka mashambani na bidhaa za viwandani kutoka mijini kupungua," anasema.

MBUNGE AJIELEZA

Je, kuna ishara gani ya kutumia aliyoyanena Waziri Mkuu Majaliwa, miaka mitano iliyopita? Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, anatoa maoni yake:

"Kabla ya Tarura kuifungua Halmashauri ya Ushetu kwa barabara zinazopitika kwa vipindi vyote vya mwaka hali ilikuwa ngumu sana.

"Tulikuwa tunalima, tunavuna sana lakini wakati mwingine unakuta tumbaku, mahindi pamoja na alizeti zetu zinakwama kutoka shambani, hivyo wakati mwingine wakulima kuuza mazao yao kwa bei rahisi ili kukwepa adha ya usafiri,"anasema

Anafafanua kwamba wakulima walikuwa wanatumia gharama kubwa ya kusafirisha mazao na hasa kipindi cha mvua, kwa sababu magari makubwa hayakuweza kuingia vijijini kuchukua mazao yao, kwa kuwa barabara zilikuwa za udongo, hata magari mengi hasa ya uzito mkubwa yanazama.

"Ilikuwa inatubidi tukodishe magari yenye uzito mdogo kwa ajili ya kusomba mazao kutoka shambani, kitu ambacho kilikuwa kikiongeza gharama za mazao huku, wakulima wengi wakishindwa kuzimudu," anasema.



Daraja la chuma lililoko Kibiti, Mkoa wa Pwani, kazi inayofanywa na TARURA.

**BOSI MKUU**

Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA), Victor Seff, anasema lengo kuu la kuanzishwa TARURA ,ni kufanya matengenezo endelevu ya barabara na madaraja kwa gharama nafuu, ili kusaidia maendeleo ya kiuchumi ya kijamii nchini.

"Wakala huu umeanzishwa ukiwa na dira ya kuwa taasisi inayoongoza katika menejimenti ya mtandao wa barabara za vijijini na mijini kwa kupanga, kusanifu na kujenga kwa kuzingatia ufanisi wa gharama," anasema.

Seff anasema, TARURA ilipoanzishwa ilikuwa na mtandao wa barabara wenye urefu wa km 108,946.19, kati ya hizo, kilomita 56,624.59 zilizotangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali ni kilomita 52, 321.60.

Anasema walifanya utambuzi na uhakiki wa mtandao wa barabara za wilaya, ikiwa ni pamoja na kilomita 52,321.60 zilizokuwa hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali na wakakamilisha.

Anasema, katika kipindi cha miaka mitano mtandao wa barabara wanazohudumia sasa una urefu wa Km 144,429.77 na zote zimeshatangazwa kwenye Gazeti la Serikali la Juni 25, 2021.

"Mtandao huo wa barabara ni ongezeko la kilomita 87,805.17 ambazo bado zilikuwa hazijatangazwa kwenye Gazeti la Serikali," anasema.

Anasema, mtandao una madaraja 3,191 na makalavati 69,317, barabara za lami km 2,404.9, za changarawe kilomita 29,166.57 na barabara za udongo km 112,858.3.

Seff anasema, fedha kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa majukumu ya TARURA zitatokana na mapato yatokanayo na huduma zinazotolewa na wakala, serikali kuu, mfuko wa barabara na wadau wa maendeleo.

Anataja wadau hao ni Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID), Shirika la Misaada la Marekani (USAID) na Umoja wa Ulaya (EU). Pia, anasema mamlaka za serikali za mitaa hutoa fedha za ujenzi na matengenezo kupitia mapato yao ya ndani.

Mhandisi Seff anasema, mpango mkakati wa kwanza wa TARURA ulianza kutekelezwa Julai Mosi, 2017 na kukamilika Juni 30, mwaka jana.

"Katika kipindi hicho, kuna barabara zenye urefu wa kilomita 24,979.24 zilifanyiwa matengenezo, kilomita 955.35 zilijengwa kwa kiwango cha lami na km 16,857.82 zilijengwa kwa kiwango cha changarawe," anasema.

Pia, anayataja madaraja 231 yaliyojengwa kutoka madaraja 2,960, hadi 3,191 sambamba na makaravati 1,325 yamejengwa.

Katika kipindi hicho anasema ukusanyaji wa mapato yatokanayo na tozo ya maegesho ya magari kwenye matumizi ya hifadhi ya barabara mapato yalifika Sh bilioni 50.41 toka Julai 2018 hadi Juni 2021.

Mtendaji huyo wa TARURA, anasema kutokana na changamoto zilizojitokeza wakati wa ukusanyaji mapato ya maegesho, TARURA ilianzisha mfumo wa kielektroniki wa Tarura Revenue Management Information System (TARMIS).

Anasema, ni mfumo uliotengenezwa na wataalamu wa TARURA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tamisemi, pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango, sasa unaonyesha mafanikio makubwa.

Seffa anaoredhesha mafanikio zaidi katika miaka mitano anasema wameweza kuwa na jengo la makao makuu katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambalo tayari linatumika,akitaja mwaka 2019 walisimika mfumo wa malipo serikalini (MUSE).

Anasema, umesaidia kuongeza udhibiti na usimamizi wa rasilimali fedha, ikiwa ni pamoja na kupunguza gharama za uendeshaji na kudhibiti matumizi ambayo hayakuwapo kwenye mpango.

Mhandisi Seff anasema, kitengo cha usanifu na usimamizi wa utekelezaji wa kazi za barabara na madaraja kiitwacho TARURA Engineering and Environmental Consulting Unit, mpaka sasa kimefanya usanifu wa barabara zenye urefu wa km 147.47 na madaraja 39.

Anasema, katika kuboresha makao makuu ya nchi, TARURA katika mji wa Magufuli, Mtumba wamejenga barabara za lami nzito zenye urefu wa km 51.2 kwa Sh 89,112,145,500.06.

**MPANGO MKAKATI ll**

Baada ya kuisha mpango mkakakti wa kwanza (2016/2017 - 2020/2021), Seff anasema TARURA imeandaa mpango pili wa miaka mitano kuboresha barabara za wilaya, yaani 2021/2022 hadi 2025/2026, ukihusisha utunzaji barabara zilizo katika hali nzuri na za wastani kubaki katika hali hiyo.

Pia, anataja itahusisha kupunguza barabara zenye hali mbaya na kuziweka katika hali nzuri, ili zipitike mwaka mzima, kukiwa na matarajio mtandao kwa barabara za lami miaka mitano ijayo utaongezeka.

Hapo kunatajwa kutoka kilomita 2,404.90 za sasa hadi kilomita ,855.65, changarawe kutoka kilomita 29,116.57 hadi 102,358.14 na madaraja idai yake 2,812, hadi 6,620 na fedha zitakazotumika kwenye mpango huo wa pili zinakadiriwa kuwa Sh trilioni 3.6.

Mratibu Humphrey Kanyenye, anayesimamia miradi hiyo chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa Fedha za Benki ya Dunia, akifafanua wana mradi wa barabara kwa ajili ya kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii nchini baadhi ikitekelezwa na TARURA.

Mradi huo ulianza Julai Mosi mwaka jana na unatekelezwa kwa miaka sita kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 350, Dola milioni 300 zikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia na Dola milioni 50 ni mchango wa serikali.

Mradi huo anasema utahusisha ujenzi wa barabara za km 535 kwa lami huku barabara za km 400 zikiwa chini ya TARURA na kilomita 135 zitakuwa chini ya Wakala wa Barabara (TANROADS).

Mradi huo pia unafanya matengenezo sehemu korofi zenye urefu wa km 2,900 pamoja na matengenezo ya kawaida urefu wa km 23,000 katika barabara za TARURA.

Maeneo yatakayonufaika na mradi huu ni barabara ya Wenda - Mgama kilomita 9 na Mtilili - Ifwagi kilomita 14, katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa na Mufindi Mtawalia.

Anasema, katika halmashauri tatu wanatekeleza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilomita 50 za mwanzo kwa kila halmashauri za; Ruangwa, Mbogwe na Handeni ambazo zina mgao wa kilomita 100 kila moja.

Kanyenye anasema, mwaka uliopo wa fedha wanatarajia kuanza ujenzi katika Bonde la Mto Msimbazi, Dar es Salaam, pakitengewa Dola za Marekani milioni 270.

Anasema mradi utahusisha ujenzi wa daraja eneo la Jangwani, mfereji na barabara yake, kwamba usanifu umeshafanyika na tathmini ya mazingira vimeshafanyika.

"Vilevile tunatarajia kutekeleza mradi mkubwa wa kuendeleza miji 45 (TACTIC). Awamu ya kwanza tunatarajia kuanza na miji 12 ya mwanzo ya Arusha, Dodoma, Tabora, Kigoma Ujiji, Mwanza Ilemela, Geita, Kahama, Morogoro, Mbeya, Sumbawanga na Songea. Utekelezaji wake umeshaanza," anasema.



Sehemu ya barabara iliyojengwa na TARURA mkoani Mbeya. **PICHA ZOTE: TARURA.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# LATRA mnaupiga wote, lakini pigeni na hapa



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
jkulangwa@yahoo.com

NAONA Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) inajaribu kuupiga mwingi. Au mnaonaje wenzangu (kwa sauti ya Uhuru K.)?

Ukifuatilia kinachofanyika, utaona inahamisha watu kutoka analogi kwenda digitali, sasa tunatakiwa tukate tiketi kwa njia ya mtandao tukitaka kusafiri kwa mabasi.

Haitoshi, naiona LATRA tofauti na iliyokuwa ile SUMA+TRA, hii inataka sasa watu wakisafiri wasafiri kwa raha bila usumbufu, kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine.

Nimewasikia wakikemea tabia ya watu kupanda kwenye mabasi na kuanza kuhubiri neno la Mungu. Pia, wale wapandao na makasha yaliyosheheni vyakula na vinywaji wakinuka vikwapa na kuhanikiza kwa abiria kununua, bei yao sasa!

Nimeyafurahia haya matatu na ndiyo sababu nadiriki kusema inajaribu kuupiga mwingi, lakini kinachotakiwa ni elimu na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa yote haya.

Najiuliza, hivi wajameni (kwa sauti ya Uhuru K.), hii digitali itawahusu na wale ndugu zetu, wazee wetu walioko vijijini na hata wasio na simu au kompyuta? Elimu imeshaanza pia huko?

Tukiambizana kuwa mwisho wa mwezi huu ndio mwisho wa tiketi analojia, tutakuwa tumetenda haki mpaka kwa hao wenzetu wa nilikokusema huko vijijini? Kama utafiti na upembuzi yakinifu umeshafanyika na kuona inafaa basi na ifae, ianze.

Na tutakapoanza, tukumbuke pia kuna wenzetu wanaopandia njiani ambao naamini hawatakuwa kwenye digitali, lakini wapo wenye dharura ya safari mara moja, kuwa limezuka la kuzuka wanataka usafiri na wako njiani huko, wanafanyaje wawe kidigitali?

Hilo kwa kweli, linahitaji elimu haina mwisho, ili kila mmoja aweze kujua jinsi ya kufanya mpaka mambo yawe barabara. Ni utaratibu mzuri tena wa kisasa, usio na usumbufu, lakini shaka yangu ni katika utekelezaji.

Lakini, kwa kuwa mwelekeo umeshaonekana hakuna linaloshindikana chini ya jua. Ili mradi kodi ya serikali inapatikana.

Tuache hilo, nirudi kwenye hawa jamaa wahubiri ndani ya mabasi mpaka kwenye daladala, wanaodhani katika mabasi abiria wote ni waumini wao! Hili la kuwazuia ni mwafaka na swadakta kabisa.

Waacheni watu waende kwenye majumba yao ya ibada, badala ya kulazimishana kwenye mabasi ambapo kila mmoja ana lake analowaza, hajui siku itaishaje mara anaingia mtumishi anasikia ooh...

Mwingine anaingia na kutisha abiria, ooh bila kusikia neno la Mungu safari hii haitakuwa na amani, hivyo sote tufumbe macho tuiombee safari yetu, kana kwamba watu walimsubiri yeye ndipo wamwombe Muumba wao, Kwani hawakuomba majumbani mwao? Wengine wakimaliza wanaomba sadaka!

We unavamia basi unawavuruga tu na utumbo street wako walahi! Hapo LATRA mmeupiga wote kabisa. Pia, wenye mabasi nao waache ile ya kutuwekea kanda za video za kiimani safari nzima, huku si wa imani tukilazimika kusikiliza.

Lingine ambalo sasa LATRA mnapaswa kuliangalia, ni hili la sisi abiria wa mikoani kulazimishwa kwenda kula kwenye hoteli za wenye mabasi au maswahiba zao kwa bei ya kuua mtu.

Abiria huna hili wala lile, mara ghafla basi linachepuka barabara na kuegesha kwenye hoteli na mnatangaziwa abiria dakika 10 za kula na kuchimba dawa, mnakwenda kula bei ni kama mkosi sijui nchi gani, tofauti kabisa na tulikozoea kwa mama/baba n'tilie.

Mnalazimika kula kwa sababu hukuna jinsi wala pengine pa kupata huduma hiyo, ila kwa ruhusa ya dereva na msaidizi wake, ambao wao kula yao ni 'kitonga', hawalipi chochote zaidi ya kupeleka wateja sisi pangu pakavu, kumchangia mwenye hoteli au basi.

LATRA mkiweza kulishughulikia na hili, bila shaka mtakuwa mmeupiga mwingi kwa funga mwaka, bila kutoa nje na hakika safari zitakuwa za mustarehe, kuliko hivi sasa ambayo tuna bambikiwa vitu vingi mpaka kufika unakokwenda, umekombwa sehemu kubwa ya akiba yako.

Ila hakuna lisilowezekana kama nilivyosema hapo

UCHUMI

BAADA KUTANGAZWA RUZUKU MBOLEA...

# TFRA yaanika njia itakayopita kumfikia mkulima aliko na mapinduzi kilimo nchini

- Elektroniki kijijini; ajenda kuu ya Maonyesho 88
- Ushuhuda rasmi wa tabasamu lake Bashe bungeni

**Renatha Msungu, DODOMA**



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA) Dk. Stephan Ngailo akipewa maelezo kutoka kwa Ofisa wa kampuni inayotoa mikopo ya mbolea kwa wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi.

MBOLEA inajulikana ni kati ya viuatilifu muhimu kwa wakulima wa mazao mbalimbali nchini, kutokana na inavyosaidia kukuza mazao, pale inapotumika ipasavyo katika sehemu husika.

Hiyo imo katika sababu zilizoifanya serikali kutenga Sh. bilioni 150, kwa ajili ya kutoa mbolea za ruzuku katika bajeti iliyoanza mwezi huu na katika kutekeleza hilo nchini, kuna Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA).

Mamlaka hiyo, kimsingi ni chombo kilichopewa dhamana kisheria kusimamia na kudhibiti mbolea, ili kuhakikisha mkulima anapata mbolea sahihi na kwa wakati sahihi, ikiwemo kwenye bei himilivu.

Kuelekea maadhimisho ya siku ya wakulima kitaifa, maarufu Nanenane ambayo kitaifa safari hii imepangwa mkoani Mbeya, TFRA imenuia kutumia mkusanyiko huo kuwapa somo wakulima, ilivyojipanga katika msimu ujao wa kilimo kuwapatia wakulima, mbolea za ruzuku .

Ndani ya hilo, kuna suala la kuhakikisha inawafikia kwa wakati ili waweze kuitumia mbolea hiyo kwenye msimu wa kilimo. Dira ya TFRA ni kuhakikisha usalama wa chakula kwa wananchi na Taifa unakuwepo, kulingana na walivyojiandaa kuwapatia wakulima mbolea nchini kote.

Hilo linatokana na uamuzi wa serikali kuwekeza zaidi kwenye sekta ya kilimo ambayo hata katika bajeti ya mwaka uliopo wa fedha, kiasi kikubwa cha bajeti kimeelekezwa huko, ikizingatiwa kilimo ni mwajiri wa sehemu kubwa ya umma.

Miongoni mwa sababu zilizotolewa, inajumuisha chombo TFRA kusaidia kupunguza makali ya bei ya mbolea, ambayo imepanda kwenye soko la dunia, kutokana na sababu tofauti.

### WANENVAVYO TFRA

Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephano Ngailo, anasema ili kuhakikisha wakulima wanapata mbolea sahihi, wamepanga kuhakikisha kuwa mzalishaji au mwingizaji wa mbolea nchini anadhibitiwa.

Hapo, azma ni kutaka mkulima atumie mifuko maalumu kwa ajili ya ruzuku yenye maandishi yanayosomeka kuhusu ruzuku, ili kuwatambulisha wakulima wanaotumia mbolea inayonunuliwa kwa bei ya ruzuku.

Dk. Ngailo anasema, wanafanya hivyo kuhakikisha wakulima wote wanapata mbolea kwa bei ya ruzuku, hata ikawasaidie kujiinua kiuchumi wao na familia zao kwa ujumla.

Anafafanua, lengo la serikali sasa ni kuona kila mkulima anafikiwa na mbolea kwa msimu wa kilimo uliopo, 2022/2023 na anasema uingizaji mbolea kwa pamoja kupitia TFRA sio jambo geni.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa TFRA, kilichopo sasa kimaendeleo ni maboresho ya mifumo ya kutoa mbolea, ili kuondoa mianya ya ubadhirifu na kuwepo kwa tija inayomfikia mkulima mnufaika wa ruzuku.

Namna usajili utakavyofanyika, Dk. Ngailo anaeleza ni kupitia ofisa ugani mahali wakulima walipo, kuanzia kata na vijiji na mdhibiti wao ni Mwenyekiti wa Kijiji, baadaye taarifa za mkulima zinaingizwa kwenye mfumo wa kielektroniki kuwezesha usambazaji wa mbolea hizo.

Anaongeza kuwa, mzalishaji au mwingizaji mbolea nchini atatumia mifuko maalum kwa ajili ya ruzuku, ili kutambulisha mbolea hiyo inayonunuliwa na mkulima kwa bei ya ruzuku.

Anasema utoaji ruzuku za mbolea si jambo jipya nchini, kwani serikali imeendelea kuboresha mifumo ya utoaji mbolea hizo, ili kuondoa mianya ya ubadhirifu hata kumfikisha mkulima aweze kunufaika vilivyo na ruzuku hiyo.

Mkurugenzi huyo anasema, wakiwa mamlaka ya mbolea kitaifa, wamejipanga kuhakikisha wakulima wananufaika na mbolea inayotolewa kwa ruzuku ya serikali na kuwataka wakulima wajiweke sawa kuhakikisha wanaifikia TFRA, kufahamu upatikanaji mbolea za ruzuku.

Anasema utoaji ruzuku za mbolea, ni matokeo ya maono ya Rais Samia Suluhu Hassan katika umuhimu wa kuwawezesha wakulima wafikie tija na uhakika wa mavuno ya chakula na kibiashara kwa, ustawi wa umma na taifa.



Shamba darasa ambalo mbolea inatumika mkoani Iringa.
**PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mchumi Mwandamizi na Kaimu Meneja wa TFRA Elizabeth Bole, anafafanua kwamba mkulima mnufaika wa mbolea ya ruzuku, ni anayesajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki, kukiwamo taarifa zake.

Ni taarifa zinazojumuisha; jina la mkulima, kijiji anachoishi, na ukubwa wa shamba lake, hali ambayo Mchumi Elizabeth anaitaja itasaidia kutoa picha halisi ya kiasi cha mbolea kinachohitajika shambani.

Anasema, lengo la TFRA ni kudhibiti ubora kwenye biashara ya mbolea, ndani ya mnyonyoro wa thamani wa uzalishaji na uingizaji wa mbolea kutoka nje, kuhifadhi usambazaji na uuzaji wake.

Elizabeth anafafanua kuwa wanatarajia baada ya maonyesho ya Nane Nane jamii na wadau mbalimbali watakuwa na uelewa sahihi wa namna ya upatikanaji mbolea za ruzuku.

### WAZIRI WA KILIMO

Waziri mwenye dhamana ya kilimo, Hussein Bashe, anaeleza dira ya mkakati uliopo nchini, ni kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika mifumo ya ruzuku iliyopita, kujikita katika elektroniki kusajili waingizaji, wasambazaji na wauzaji mbolea, ili kuwahakikishia wakulima wanufaika na mbolea.

Bashe anasema, mfumo huo uliowekwa utatumika katika kuhakikisha huduma zote za usambazaji mbolea za ruzuku zinatolewa na mtu sahihi na kumfikia mkulima mwenyewe na si vinginevyo.

Waziri Bashe anasema kuwa ajenda ya sasa ni kuzama katika kilimo cha biashara, hapo kunaibuka haja ya umuhimu wa Sensa , kwani itawasaidia watu kuhesabiwa kwa mipango bora katika sekta ya kwenye kilimo, mifugo na uvuvi nchini.

Anadokeza ni sehemu ya msingi unaoifanya serikali kuwa na kila sababu ya kuhakikisha inawekeza nguvu kubwa katika sekta ya kilimo, kumuona mkulima anapiga hatua katika safari ya kutafuta kilipo kilimo biashara.

### NENO LA WAKULIMA

Muhina Njelwa, ni mkulima anayeisifu serikali, akipongeza kwa kauli 'imefanya jambo kubwa' kwa ajili ya sekta ya kilimo, akiwataka wakulima wenzake kuchangamkia fursa za kutembelea banda la TFRA katika maonyesho ya Nanenane, wapate elimu stahiki ya upatikanaji mbolea za ruzuku, kwa bei ya serikali.

Anasifu kuwa wamejengea mazingira bora ya kilimo, hata kufunguliwa mazingira bora ya safari kuingia kwenye kilimo cha biashara.



# Vijana 800,000 waingia soko la ajira

Na Augusta Njoji, DODOMA

IMEELEZWA kuwa kila Mwaka takribani vijana 800,000 wanaingia katika nguvu kazi ya Tanzania wakiwa na matarajio madogo ya kupata ajira.

Kutokana na hali hiyo, imeshauriwa kuwapa vijana ujuzi, mafunzo na rasilimali wanazohitaji kuchangia uchumi wa nchi.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Misaada la Marekani(USAID), Kate Somvongisiri, alibainisha hayo juzi kwenye ufungaji wa mradi wa Feed the Future Tanzania Inua Vijana uliotekelezwa kwa ufadhili wa USAID kwa miaka mitano (2017-2022).

"Ili Tanzania ipate manufaa ya ongezeko la idadi ya vijana na kufikia malengo ya ajenda yake ya maendeleo, ni muhimu zaidi kuliko wakati mwingine kuwapa vijana ujuzi," alisema

Mkurugenzi huyo alisema asilimia 67 ya nguvu kazi ya Tanzania inajishughulisha na kilimo ili kukabiliana na ukosefu wa ajira, serikali na wadau wanapaswa kuhimiza ushirikishwaji wa vijana kwenye sekta hiyo.

Akizungumzia mradi huo, alisema mpango huo umewafikia zaidi ya vijana 43,000 na kutoa zaidi ya Sh. Bilioni 5.3 kama ruzuku kwa shughuli za biashara na kilimo zinazomilikiwa na vijana.

Mradi huo, alisema umebadilisha mtazamo wa jamii kuhusu vijana na kuwa mawakala wa maendeleo wenye uwezo wa kubadilisha jamii inayowazunguka.

Akifunga mradi huo, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, aliziagiza wizara na taasisi zinazohusika na ustawi wa jamii kuja na mpango mkakati wa kushughulikia kero zinazowakabili vijana nchini.

Alisema serikali itaendelea kuwekeza katika maendeleo ya vijana na maeneo mengine yenye lengo la kuleta usawa kwa wananchi.

Pia alisema agizo lingine la Waziri Mkuu ni kwa mamlaka za serikali za mitaa zihakikishe zinawatambua na kuwapatia mikopo vijana hao.

"Agizo lingine ni Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi Ajira na Wenye Ulemavu ishirikiane na Ofisi ya Rais-TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa) kuhakikisha vijana wanaendelea kuwezeshwa na kujengewa uwezo na kupewa vitendea kazi," alisema.

Prof. Ndalichako alitoa rai kwa vijana walionufaika na mradi huo kuhakikisha wanaendeleza mafanikio mazuri ya mradi.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo, akishiriki kupanda miti kwenye Shule ya Feza, jijini Dodoma mapema wiki hii, baada ya kushiriki mbio za hisani, zilizoandaliwa na shule hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Serikali yahimiza kasi ujenzi kituo

Na Renatha Msungu, DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Kaspar Mmuya, amemwagiza mkandarasi anayejenga Kituo cha Uratibu na Udhibiti wa Maafa eneo la Nzuguni, jijini Dodoma, kuongeza kasi ili kukamilisha kazi kwa wakati.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho, Mmuya alisema ujenzi wa kituo hicho unaogharimu zaidi ya Sh. bilioni mbili, unapaswa kuwa na ubora kulingana na thamani ya fedha.

"Licha ya changamoto ndogo ndogo zilizopo katika mradi huu, ni vizuri mkandarasi akaongeza speed (kasi) ya ujenzi wa mradi huo.

"Ni vizuri kutumia kipindi ambacho hakina changamoto nyingi kufanya kazi nyingi kwa uharaka ili changamoto zikija zile ambazo huwezi kuzikabili inakuwa rahisi kukamilisha ujenzi huo,"alisema Mmuya.

Alisema lengo lao ni kuona kituo hicho kinakamilika kwa wakati na kuanza kufanya kazi kama yalivyo matarajio ya serikali.

Pia Alimtaka mkandarasi kuongeza nguvu ya ujenzi wa kituo hicho ikiwamo vifaa na muda wa kufanya kazi.

"Naomba mtekeleze kazi yenu kwa weledi. Wito wangu muongeze kasi ili serikali izidi kuwaamini na

# Kampuni Uswisi kuwekeza biashara ya hewa ukaa

Na Mwandishi Wetu, DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo amekutana na wawekezaji wa kampuni ya Black River kutoka Uswisi wenye lengo la kuwekeza katika biashara ya hewa ukaa.

Akizungumza kuhusu kikao hicho jana, Dk. Jafo aliahidi kushirikiana na wadau wa mazingira katika kuhakikisha Tanzania inanufaika na biashara ya hewa ukaa.

Waziri huyo alisema katika Mkutano wa 26 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP 26) uliofanyika Glasgow, Scotland, mwishoni mwa mwaka jana, miongoni mwa agenda kubwa iliyopewa msukumo madhubuti ni pamoja na namna ambavyo nchi zitakavyonufaika na biashara ya hewa ukaa.

"Tunaweka misingi mizuri ya kuhakikisha sasa Tanzania inanufaika na biashara ya hewa ukaa kwa kukamilisha mwongozo wa biashara hiyo," alisema.

Aliagiza timu ya wataalamu kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Ofisi ya Rais TAMISEMI (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara ya Fedha na Ofisi ya Maliasili na Utalii kuchakata andiko litakalowasilishwa na kampuni ya Black River ndani ya wiki mbili.

"Ni matumaini yangu kuwa biashara ya hewa ukaa itaweza kusaidia katika bajeti kubwa ya Serikali, kuelekea bajeti ya mwaka 2023/24 nchi inufaike na biashara hii huku tukilinda mazingira," alisema.

"Pamoja na ukweli kwamba Tanzania sio miongoni mwa nchi zinazozalisha gesi joto kwa wingi duniani. Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imechukua hatua za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zikiwamo kujenga uwezo wa kitaasisi, kutoa elimu kwa jamii na kuhimiza shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi," aliongeza.

Mkurugenzi Mkuu wa Black River, Cedric Biart, alisema kampuni yake iko tayari kuwekeza nchini, kunufaisha wananchi kupitia makubaliano na ushirikiano baina ya serikali kuu, serikali za mitaa na wananchi wanaozunguka hifadhi za misitu katika jitiihada za kuhifadhi mazingira.





# Mwanafunzi ashikiliwa tuhuma kukutwa na risasi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia mwanafunzi wa kidato cha nne, Shule ya Sekondari ya Wazazi ya Mbalizi, Leodiga Mbunda (17), kwa tuhuma za kukutwa na risasi ya silaha za kivita akiwa ameiweka mfukoni.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema mtoto huyo alikamatwa Julai 27, mwaka huu katika maeneo ya Mtakuja, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi akiwa na risasi hiyo ambayo inadaiwa kuwa ni ya bunduki aina ya AK.47.

Alisema alikamatwa asubuhi wakati wa msako maalumu uliofanywa na makachero wa jeshi hilo kwenye maeneo mbalimbali ya mji huo na walipomkamata walimpekua na kukuta ameificha kwenye mfuko wa koti.

Alisema bado haijajulikana aliikuta wapi risasi hiyo na alikuwa anaenda kuifanyia nini kama asingekamatwa, jeshi hilo linaendelea kumhoji ili kujua alikoitoa.

"Bado tunaendelea kumhoji ili tujuwe alikoitoa na alichokuwa anataka kuifanyia risasi hiyo, tukio hili sio la kawaida, lakini tunaamini kuwa tutapata ukweli wa jambo hili," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linawashikilia watu 14 raia wa Rwanda kwa tuhuma za kuingia nchini bila kuwa na vibali.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa Julai 24, mwaka huu saa 1:45 jioni katika kizuizi cha Polisi cha Chalangwa kilichopo wilayani Chunya na maaskari waliokuwa doria.

Alisema kati ya watuhumiwa hao, 11 ni wanaume, mmoja ni mwanamke na wawili ni watoto, na walikuwa wanasafiri kwenye basi lenye namba za usajili T.860 BDR mali ya Kampuni ya Hamed Prince.

Watu hao walipanda kwenye gari hilo kama abiria wa kawaida na walikuwa wanatokea mkoani Tabora kwenda Mbeya na hatimaye kuelekea nchini Malawi.

Kamanda Matei aliwataka wananchi na viongozi wa serikali za mitaa kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa taarifa za viashiria vya uhalifu huku akisisitiza kuimarisha vikundi vya ulinzi shirikishi kwenye maeneo yao.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete (kushoto) na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Rungwe, Sam Mwakapala (katikati), wakishiriki kwenye ujenzi wa Zahanati ya kijiji cha Ngeleka, kata ya Kisegese, Halmashauri ya Busokelo, wilayani humo juzi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# REA yapewa miezi minne kukamilisha usambazaji umeme

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

SERIKALI imetoa miezi minne kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA), kukamilisha usambazaji wa umeme katika Kijiji cha Itumbi, Kata ya Matundasi, Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya ikiwamo kwenye migodi ili kuinua shughuli za kiuchumi.

Waziri wa Nishati, January Makamba alitoa agizo hilo juzi alipofanya ziara katika kijiji hicho na kupata malalamiko kwa wananchi kuwa mpaka sasa hawajaunganishiwa huduma hiyo na baadhi ya shughuli zao kukwama.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Masache Kasaka, alisema kijiji cha Itumbi ndicho kinachoongoza katika wilaya hiyo kwa kuwa na migodi mingi ya dhahabu, lakini hakijawahi kuwa na umeme tangu kilipoanzishwa.

Alisema wachimbaji wanalazimika kutumia mafuta ya dizeli kwenye migodi hali ambayo alisema inaongeza gharama za uzalishaji na hivyo akamuomba Waziri kuwasaidia wachimbaji hao kupata huduma hiyo muhimu.

Alisema mbali na kwenye migodi, lakini pia maeneo mengi ya kijiji hicho wananchi bado hawajaunganishiwa umeme licha ya kijiji kuwa tayari na nishati hiyo.

"Hapa mheshimiwa waziri wananchi wengi hawana umeme na shughuli zao nyingi zinakwama, kuna kijiji hapa kinaitwa Matondo, wananchi wanaona tu nyaya zimepita, lakini hawajaunganishiwa huduma hii nao tunaomba waunganishiwe," alisema Masache.

Alisema endapo wananchi hao watakuwa wameunganishiwa nishati hiyo, shughuli zao za uchumi zitaongezeka na hata uzalishaji wa dhahabu utaongezeka kutokana na gharama za uzalishaji kupungua.

Baada ya maelezo hayo, Waziri Makamba, aliwataka watendaji wa REA, makandarasi na maofisa wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Mkoa wa Mbeya kutoa ufafanuzi kuhusu kero hiyo.

Msimamizi wa miradi ya REA nchini, Hamis Mrope, alisema wametenga bajeti ya Shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kujenga njia ya umeme wa msongo wa kati wenye urefu wa kilomita 19 na huo ndiyo utasaidia kupunguza tatizo la umeme kijijini hapo. Alisema pia, wametenga zaidi ya Sh. milioni 200 kwa ajili ya kujenga njia ya umeme wa msongo mdogo wenye urefu wa kilomita sita kwa ajili ya kusambaza kwenye makazi ya wananchi wasiopungua 150. "Tulishafuatilia na kubaini kwamba katika kijiji hiki kuna mahitaji makubwa ya umeme kwa hiyo naomba niwatoe hofu wananchi wa hapa kwamba watapata huduma hii ndani ya miezi miwili ijayo," alisema Mrope.

Alisema wapo makandarasi wanaoendelea na kazi mbalimbali za miradi ya kuunganisha umeme kwenye vijiji pamoja na miradi ya ujazilizi kwenye maeneo ambayo nishati hiyo ilishafika, lakini wananchi hawajaunganishiwa.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Mathias Solongo, alisema mbali na miradi hiyo pia shirika hilo limetenga zaidi ya Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya kusambaza umeme kwenye migodi ya dhahabu iliyopo kijijini hapo.

Alisema baada ya miradi hiyo kukamilika wananchi wa wilaya maeneo hayo watakuza shughuli za kiuchumi hasa kwenye migodi ambako alisema sasa hivi wapo kwenye hatua nzuri za ukamilishaji.

Waziri Makamba aliagiza mpaka kufikia mwezi Desemba wawe wamekamilisha miradi yote ya usambazaji wa nishati hiyo kwa wananchi na ikishindikana wanatakiwa kukamilisha kabla ya mwezi Februari.

Aliutaka uongozi wa wachimbaji wa dhahabu katika wilaya hiyo kumpelekea taarifa endapo hawatapatiwa huduma hiyo kwenye maeneo hayo.

# MUST yapatiwa msaada vifaa vya kujifunzia

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAASISI ya Afya ya Ifakara kupitia programu ya Nest 360 Tanzania imetoa msaada wa vifaatiba vya kulinda afya za watoto wachanga vya kujifunzia Sayansi ya Vifaatiba katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), vyenye thamani ya Sh. milioni 70.

Vifaa hivyo vimetolewa katika chuo hicho ili kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa wanafunzi wa fani hiyo ya ukarabati wa vifaa tiba ambayo ni mpya katika chuo hicho na huzalisha wataalamu ambao watalisaidia taifa kupunguza uagizaji wa mafundi nje ya nchi.

Akikabidhi vifaa hivyo juzi, Mratibu Kiongozi wa Mradi wa Nest 360, Donat Shamba, alisema taasisi hiyo imelenga kutoa msaada wa aina hiyo kwenye maeneo mbalimbali nchini na kwamba kwa kanda ya Nyanda za Juu Kusini kituo kinachonufaika ni MUST.

Alivitaja vituo vingine vitakavyonufaika kuwa ni Arusha, Dodoma, Mwanza kupitia hospitali ya Bugando na Dar es Salaam kupitia Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT).

Shamba alisema taasisi hiyo iliitoa msaada huo baada ya kubaini uwapo wa tatizo la uhaba wa wataalamu wa vifaa vya kulinda ya watoto wanaozaliwa.

"Vifo vya watoto wachanga vimekuwa vikiongezeka katika maeneo mengi nchini licha ya kwamba kwa sasa upo utaalamu mkubwa wa kuokoa maisha ya vichanga hivyo, sasa tunaamini kwamba vifaa hivi vitazalisha wataalamu ambao watakuwa wanakarabati vifaa hivi vinapopata shida," alisema Shamba.

Mhandisi wa vifaa tiba wa programu ya Nest 360 Tanzania, Elizabeth Ngowi, alivitaja vifaa vilivyotolewa katika chuo hicho kuwa ni mashine ya kutibu watoto waliozaliwa na tatizo la manjano ya ngozi na mashine ya joto kwa watoto wanaozaliwa kabla ya muda.

Vifaa vingine ni mashine ya kusaidia kufungua mapafu ya mtoto mchanga ili aweze kupumua vizuri, mashine ya Oksijeni, ya kutoa vitu visivyotakiwa katika mwili wa mtoto anapozaliwa na ya kuangalia kiwango cha oksijeni kinachoingia mwilini.

Akipokea vifaa hivyo, Naibu Makamu Mkuu wa MUST, Prof. Godliving Mtui, alisema msaada huo utakuwa chachu ya kuzalisha wataalamu wengi watakaokwenda kusaidia maisha ya watoto wachanga nchini.

Aliishukuru tasisi hiyo ya afya Ifakara kwa msaada huo na kwamba wadau wengine wa afya wanatakiwa kuiga mfano wa taasisi hiyo kutambua umuhimu wa uzalishaji wa wataalamu wa vifaa tiba.

Alisema chuo hicho kimeanza kuzalisha wataalamu wa ukarabati wa vifaa tiba, lakini tatizo lililopo ni upatikanaji wa ajira kuwa mgumu kutokana na kuwa ni fani mpya nchini.

"Wadau wengi hawatambui uwapo wa wataalamu hao, kwa hiyo tuna kazi ya kuanza kuipigia kampeni fani hii na kuwatangaza wahitimu wetu ili waajiriwe," alisema Prof. Mtui.



## HABARI ZANZIBAR

# Wafugaji wakabiliwa ukosefu vifaranga samaki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

USHIRIKA wa ufugaji samaki na ukulima wa chumvi wa kijiji cha Pujini, Mkoa wa Kusini Pemba (Kibaridi fishing farm), umesema kuwa fedha na nguvu nyingi wanatumia katika kazi hiyo lakini wanakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo kukosa vifaranga vya samaki.

Hayo yalielezwa na Mwenyekiti wa ushirika huo, Ahmed Salum Issa, wakati akitoa taarifa kuhusu ufugaji wa samaki na ukulima wa chumvi wakati Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alipofika kijijini hapo kujionea shughuli za ufugaji.

Mwenyekiti huyo alisema licha ya juhudi zao za kuunga mkono kwa vitendo azma ya serikali ya uchumi wa buluu, changamoto kuu ni kukosa vifaranga na soko la chumvi na kusababisha hali zao za kimaisha kuwa duni.

Alisema masikitiko yao ni kushindikana kupatikana kwa vifaranga vya samaki vya maji ya bahari jambo ambalo linawatia hasara na kuwavunja moyo kwa sababu wanafuga samaki aina ya mwatiko ambao vifaranga vyake ni vya kubahatisha.

Alisema kutokana na changamoto hiyo wana idadi ndogo ya samaki ikilinganishwa na uwezo wa shamba na wana uhitaji wa vifaranga vya samaki milioni moja na laki tano.

"Changamoto yetu mheshimiwa rais ni kukosa vifaranga vya uhakika na vyenye ubora, vifaa vya kufanyia kazi ikiwamo mashine ya kutengeneza vyakula vya samaki, za kuingiza oksijeni katika mabwawa ya samaki, elimu ya ujasiriamali, ghala la kuhifadhia chumvi, soko la chumvi na fedha za kuendesha ufugaji wa kaa na Kamba," alisema.

Alisema kutokana na kukabiliwa changamoto hizo bado hawajafikia malengo yao ya kujikomboa kiuchumi na kuondokana na umaskini.

"Lengo letu la kuanzisha kikundi hiki cha ushirika ni kutumia fursa zilizopo kwa kujiajiri wenyewe kuanzisha miradi halali ya kiuchumi kujipatia kipato halali na kuondokana na umasikini," alisema.

Naye Waziri wa Uchumi wa Buluu na Maendeleo ya Uvuvi, Masoud Suleiman Makame, alisema kuwa changamoto hizo wanazielewa na tayari wizara imeshafikia makubaliano na mwekezaji ambaye atawekeza katika uzalishaji wa vifaranga na mwanzoni mwa mwezi wa Agosti watasaini mkataba wa utekelezaji.

Alisema baada ya kusaini mkataba huo, wanategemea tatizo la changamoto ya ukosefu wa vifaranga utaondoka na wafugaji kujiandaa kwa ufugaji wa samaki.

Akizungumzia ufugaji wa samaki, alisema wana mpango wa kufuga katika maeneo yote badala ya kuzalisha chumvi kwa sababu ya kukosa soko la chumvi.

Alisema katika eneo hilo wana uwezo wa kuzalisha samaki milioni sita kwa mwaka na watakapozalisha vifaranga watakaa pamoja na washirika wao wawekezaji vifaranga vya aina zote vinapatikana ili kuinua hali za wananchi kiuchumi.

Kwa upande wake, Rais Mwinyi alisema tafsiri ya uchumi wa buluu ni kuitumia bahari kujipatia kipato na ndani yake kuna uvuvi, ufugaji wa samaki, kaa, kamba na ukulima wa mwani.

Alisema katika suala la uvuvi na ukulima wa mwani, kuna juhudi nzuri zilizofanyika ikiwamo wavuvi na wakulima wa mwani kupatiwa vitendea kazi vya kisasa na kuwa juhudi za ziada zinahitajika katika ufugaji wa samaki.

"Nimejionea mimi mwenyewe kwa kweli juhudi iliyowekwa hapa ni kubwa kwa kutumia uwezo wenu wenyewe, serikali tuna kila sababu ya kukusaidieni na hivyo tutataka wahusika kuwapatia mitaji mnayohitaji na kupatiwa vifaranga," alisema.

Aliitaka wizara husika kuhakikisha vifaranga vinapatikana kwa muda mfupi sana kwa sababu serikali inatumia fedha nyingi kutengeneza mabwawa ya ufugaji wa samaki na bila ya vifaranga ufugaji wa samaki hautafanyika.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akivua samaki katika bwawa la ufugaji samaki wa ushirika wa wafugaji wa kijiji cha Pujini, mkoa wa Kusini Pemba jana. P**ICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi aipongeza Taasisi ya Milele miradi maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Taasisi ya Milele kwa juhudi zake za kuiunga mkono serikali yake katika miradi mbalimbali ya maendeleo.

Rais Mwinyi aliyasema hayo wakati akizungumza na wananchi baada ya kukagua ujenzi wa barabara ya Kijangwani hadi Birikau, Kisiwani Pemba yenye urefu wa kilomita 4.3 inayojengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema kuwa, asasi zisizo za kiserikali ziko nyingi, lakini Taasisi ya Milele imekuwa na mchango mkubwa kuiunga mkono serikali.

Alisema, taasisi hiyo imesaidia katika ujenzi wa shule, nyumba, misikiti pamoja na miradi kadhaa ya maendeleo.

Pia, alisema ukamilishaji wa ujenzi wa barabara hiyo fedha zake zimeshatiwa kwenye bajeti ya mwaka huu.

Aliwapongeza wananchi wa maeneo hayo kwa hatua waliyoichukua ya kutotaka kulipwa fidia ya mazao yao yalivyoathirika wakati wa ujenzi wa barabara hiyo.

Naye Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Mohammed, alisema katika mambo yaliyopangwa kufanywa kisiwani Pemba ni pamoja na kujenga jengo jipya la abiria pamoja na njia ya kurukia na kutulia ndege katika kiwanja cha ndege kisiwani humo ili ndege kufanya safari.

Alisema Bandari ya Mkoani, itajengwa ili kupokea meli za mizigo ikiwamo makontena, hatua itakayopunguza gharama kwa wananchi pamoja na ujenzi wa barabara ya Chake, Wete na Mkoani hadi Chake.

Ofisa Mdhamini wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Ibrahim Saleh Juma, aliipongeza Taasisi ya Ifraji Zanzibar Foundation pamoja na Milele kwa wazo lao la kusaidia ujenzi wa barabara hiyo ambayo ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

# Ulaji mbaya chakula tishio ugonjwa shinikizo la damu

**Na Mwandishi Wetu**

WATU milioni nane duniani hufa kila mwaka kutokana na ugonjwa wa shinikizo la damu (presha) na watu bilioni moja sawa na asilimia 26 ulimwenguni kote wanaishi na maradhi hayo kutokana na mfumo mbaya wa ulaji chakula.

Akitoa elimu kwa waandishi wa habari Mjini Unguja, Ofisa wa kitengo cha maradhi yasiyo ambukiza, Zanzibar, Dk. Lulu Omar, katika kituo cha jumuiya ya watu wanaoishi na maradhi yasiyo ambukiza kuhusu athari za maradhi ya shinikizo la damu.

Alisema, kwa mujibu wa utafiti uliofanyika mwaka 2011 Zanzibar, watu wenye umri kati ya miaka 25 hadi 65 ndiyo hupata maradhi hayo kwa kiwango kikubwa na ni chanzo kikubwa cha kupata ulemavu kutokana na ugonjwa wa kiharusi na vifo vya mapema.

Aliitaka jamii kuchukua tahadhari kwa kufanya mazoezi, kula mlo kamili wenye matunda na mboga na kupunguza vyakula vizito kabla ya kulala.

Aidha, alisema ni vyema jamii ikaacha kutumia vyakula vyenye mafuta kwa wingi, nyama nyekundu, chumvi nyingi na sukari, soda na ulevi ambavyo ni kichocheo kikubwa cha maradhi hayo.

Alisema, wagonjwa wa maradhi yasiyo ambukiza ni vyema wakafuata ushauri wa wataalamu wa afya kuliko kutumia dawa za miti shamba ambazo hazijathibitishwa.

Pia, aliitaka jamii kujenga utamaduni wa kufika vituo vya afya kuchunguza afya zao mara kwa mara kwa kuwa kufanya hivyo kutasaidia kuepukana na maradhi hayo.

Naye Meneja wa jumuiya ya watu wanaoishi na maradhi yasiyo ambukiza, Haji Khamis, aliwataka wagonjwa wa maradhi hayo kuzitumia dawa kwa mujibu wa maelekezo na ushauri wa wataalamu wa afya na kwamba kufanya hivyo kutasaidia kuishi kwa matumaini.

Alisema kwenda kinyume na ushauri wa wataalamu kutaongeza athari zaidi kwa mgonjwa wa maradhi hayo.

MKOMBOZI COMMERCIAL BANK

a bank with integrity

## MKOMBOZI COMMERCIAL BANK PLC

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa June-22 | Robo Mwaka ya /Mwaka Uliopita Mar-22 |
|---|---|---|---|
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 7,540 | 7,193 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 12,873 | 13,983 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 35,345 | 40,221 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 9,784 | 6,211 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 58 | 77 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 119 | 18 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 21,333 | 20,638 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 2,000 | 2,000 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 117,589 | 113,434 |
| 12 | Mali Nyingine | 6,098 | 5,800 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 539 | 539 |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 6,564 | 6,685 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **219,844** | **216,799** |
| | | | |
| B. | DHIMA | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 178,354 | 176,663 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 6 | 6 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 4,487 | 4,467 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 9 | 9 |
| 27 | Dhima Nyingine | 4,865 | 4,338 |
| 28 | Madeni | 4,333 | 4,431 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **192,054** | **189,915** |
| 30 | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **27,790** | **26,883** |
| C. | FEDHA ZA WANAHISA | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 22,820 | 22,820 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (777) | (1,994) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,966 | 1,059 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 3,781 | 4,997 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **27,790** | **26,883** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 2,737 | 3,028 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 11,180 | 14,124 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 3,407 | 4,264 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 13% | 12% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 9% | 12% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68% | 67% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55% | 54% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 80% | 81% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 1% | -3% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 1% | 0% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 JUNI 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa 30-06-2022 | Robo ya mwaka Linganishi mwaka uliopita 30-06-2021 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-06-2022 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-06-2021 |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| 1 | Mapato ya Riba | 5,767 | 6,305 | 12,003 | 11,996 |
| 2 | Gharama za Riba | (1,761) | (2,105) | (3,333) | (4,314) |
| 3 | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **4,005** | **4,200** | **8,670** | **7,682** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | **(692)** | (1,023) | **(1,325)** | (1,398) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **1,521** | **1,155** | **2,588** | **2,149** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 347 | 169 | 525 | 355 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 958 | 876 | 1,633 | 1,575 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 215 | 110 | 430 | 220 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,928)** | **(3,959)** | **(7,967)** | **(7,856)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (2,009) | (2,073) | (4,117) | (4,214) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (1,918) | (1,886) | (3,850) | (3,641) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **906** | **374** | **1,966** | **577** |
